

UK. 22

**KROOS AONDOKA MADRID NA TAJI LA SITA LA UEFA**

Jumatatu Juni 3, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581696

LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz

www.ippmedia.com
www.facebook.com/nipashetz

MWANGA WA JAMII
www.instagram.com/theguardian_newspaper

**Saruji** Mbeya yatoa gawio bilioni 3/- kwa serikali

UKURASA 5



**ACT:** Kinachojiri Afrika Kusini kiwe funzo kwa CCM

UKURASA 7




**Raia** Canada kizimbani shtaka la udanganyifu bil. 2/- za Patel

UKURASA 7



# Ziara ya Samia Korea yavuna trilioni 6.481/-

**KUELEKEZWA** kwenye miradi ya miundombinu; neema yashukia biashara, viwanda, usafirishaji... *Endelea Ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na mwenyeji wake Rais wa Jamhuri ya Korea, Yoon Suk Yeol, kabla ya kushuhudia hafla ya utiaji saini mikataba mbalimbali baina ya nchi hizo iliyofanyika Ikulu Seoul jana. **PICHA: IKULU**

## FRED LOWASSA:
## Nchimbi hakikisha ya baba hayajirudii ndani ya CCM

UKURASA 3



## Bunduki 91, risasi 276 zanaswa porini

UKURASA 5

**MICHEZO** DIARRA ACHAGUA KUBAKIA YANGA UK.24

**KATUNI** UK.6

# Ziara ya Samia Korea yavuna trilioni 6.481/-



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea zawadi ya CD zenye baadhi ya filamu zilizochezwa na watayarishaji maarufu wa Jamhuri ya Korea baada ya kuzungumza nao jijini Seoul juzi. Rais Samia yuko Korea kwa ajili ya ziara rasmi ya kikazi. **PICHA: IKULU**

**Na Salome Kitomari,**
SEOUL KOREA

RAIS Samia Suluhu Hassan na Rais wa Jamhuri ya Korea, Yoon Suk Yeol, wameshuhudia utiaji saini wa mkataba mmoja, Hati za Makubaliano (MoU) mbili na tamko la pamoja la kuanzisha Mkataba wa Ushirikiano wa Uchumi (EPA).

Tukio hilo lilifanyika jana katika Ikulu ya Jamhuri ya Korea katika Jiji la Seoul, wakati wa ziara rasmi ya Rais Samia kwa mwaliko wa kiongozi huyo, ikiwa ni ya pili kufanyika kwa miaka 26 baada ya Rais wa awamu ya tatu, Hayati Benjamin Mkapa, mwaka 1998.

Aidha, manufaa ya moja kwa moja kwa Tanzania baada ya kusaini kwa nyaraka hizo ni mkataba wa kuiwezesha nchi kupokea mkopo kutoka Korea wa Dola za Marekani bilioni 2.5 (Sh. trilioni 6.481) kwa kipindi cha mwaka 2024 hadi 2028.

"Fedha hizo ni kwa ajili ya miradi ya miundombinu ya maendeleo zinatolewa chini ya Mfuko wa Ushirikiano wa Maendeleo ya Uchumi wa Serikali ya Korea (EDCF). Ili kufungua milango zaidi ya ushirikiano wa kibiashara na kiuchumi, Tanzania na Korea zimesaini pia mkataba wa EPA utakaowezesha kuufanya uhusiano kuwa wa kimkakati hususan katika nyanja za biashara, uwekezaji, viwanda na usafirishaji," ilifafanua taarifa iliyotolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu.

Makubaliano hayo yana lengo la kufungua milango zaidi ya ushirikiano wa kibiashara na kiuchumi na kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi tatu barani Afrika ambazo zitafanya majadiliano hayo yatakayozaa Mkataba wa Ushirikiano wa kiuchumi na Korea, na kwamba nchi zingine ni Morocco na Kenya.

Hati za makubaliano zilizotiwa saini leo ni pamoja na Ushirikiano katika Uchumi wa Buluu ambapo Tanzania itashirikiana na Korea Kusini katika maeneo ya uvuvi, viwanda vya kuchakata mazao ya bahari, ujenzi wa bandari za uvuvi, teknolojia na utafiti wa masuala ya bahari, kwa ajili ya kuwanufaisha Watanzania kupata ajira za moja kwa moja na nyinginezo ikiwamo ukuaji wa uchumi.

Pia Wizara ya Madini ya Tanzania na Wizara ya Biashara, Viwanda na Nishati ya Korea Kusini zimetia saini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano katika Madini ya Kimkakati.

"Tanzania na Korea Kusini zitashirikiana katika utafiti, uwekezaji, uchimbaji na kujenga uwezo wa kuongeza thamani ya madini ya kimkakati nchini Tanzania. Madini hayo ni Nickel, Lithium na Kinywe," ilifafanua taarifa hiyo.

Aidha, Rais Samia amependekeza ushirikiano wa sekta nyingine mpya zikiwamo maendeleo ya nishati ya gesi asilia, sekta ya ubunifu ya sanaa na filamu; na kufunguliwa kwa soko la ajira la nchini Korea kwa vijana wa Tanzania kupitia mpango wa 'Employment Permit System' (EPS).

Ziara ya Rais Samia ni ya kimkakati kutokana na fursa nyingi zilizopo kwa Tanzania kwenye maeneo ya biashara, madini, miundombinu na mazao kwa kipindi ambacho Korea inajitanua kufungua milango kwenda Afrika na kwamba biashara kati ya nchi hiyo na dunia, Afrika inaambulia asilimia moja pekee.

Nchi hiyo ambayo ni ya 13 kwa uchumi mkubwa dunia inafungua masoko mapya kutokana na somo walilolipata wakati wa COVID-19 wakitegemea nchi za China, Japani na Urusi kupata malighafi, lakini walifunga hali iliyosababisha upatikanaji wake kuchukua muda mrefu.

Aidha, kutokana na hali hiyo walitafuta mbadala wa mnyororo wa usambazaji, huku sababu nyingine ni kufikia lengo la dunia la kuondoa hewa ukawa kwa asilimia 50 wakitaka kutumia nishati jadidifu, lakini wanakosa malighafi za betri na ndio sababu ya kuifikiria Afrika.

Pia sababu nyingine ni soko la Korea kubwa kuwa Ulaya na Marekani ambako kuna sheria kwamba ili kampuni za nchi hizo (Marekani na Ulaya) zizalishe bidhaa bila malighafi kutoka China, ndio sababu ya kutafuta uhusiano na nchi za Afrika ili kutafuta fursa.

**KWANINI TANZANIA**

Tanzania imetokea kupendwa na Korea ikiwa ni miongoni mwa nchi saba za Rwanda, Ghana, Msumbiji, Senegali, Ethiopia na Uganda.

Inaongoza kupata misaada na mikopo ya miradi nafuu baada ya Misri inayopata jumla ya Dola za Marekani bilioni 1.6 na Tanzania ikifuata kwa Dola bilioni 1.3.

Tangu kuanza uhusiano wa Tanzania na Korea mwaka 1992, kwa miaka mitano misaada iliyopokelewa mwaka 2014-2020 zilitolewa dola milioni 733 ambazo zilitumika kwenye mradi ya ujenzi wa Hospitali ya Taifa ya Mlonganzila Muhimbili, Daraja la Maragarasi, Mradi wa Vitambulisho vya Taifa (NIDA), mradi wa umwagiliaji Zanzibar.

Aidha, mwaka 2021-2025 serikali ilisaini miradi ya Dola bilioni moja, ambayo ni upimaji ardhi kwa dijitali utawekeza data za viwanja kidijitali, Chuo cha Teknolojia Kijiditali (DTI), Ujenzi wa Hospitali ya Miguni Zanzibar ya vitanda 600.

Pia kuna mradi wa Dola milioni 230 wa kuijenga upya Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), ambayo itakuwa ni maghorofa na kwamba ujenzi utaendelea huku huduma zikiendelea na hadi 2030 utakuwa umekamilika.

Miradi mingine ni Visiwani Zanzibar kitajengwa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano, Bandari ya Uvuvi Bagamoyo na Chuo cha Reli cha Kisasa, na kwaamba nyongeza ya mkopo wa Dola za Marekani bilioni 2.5.

Kutokana na mikopo hiyo Tanzania itaamua miradi ya kutekeleza na riba yake ni asilimia 0.001 utakaolipwa kwa miaka 40 na inalipwa baada ya miaka 25.

Nguvu kubwa itaelekezwa kwenye ushirikiano katika madini ya kimkakati na kwamba Tanzania imedhamiria kuweka nguvu eneo hilo kwa kupima kwa kuwa asilimia 16 pekee ndio yamepimwa kwa kuwa wana teknolojia kubwa.

Katika eneo la madini Tanzania imejipanga kimkakati kwa kuongeza thamani ya madini ili kuhakikisha wananchi wananufaika.

Eneo jingine ni kufungua uchumi wa bahari (uchumi wa blue) na kwamba Rais Samia na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, ambako Tanzania haijavuna kwa kuwa kuna samaki aina ya Jodari ambao wana soko kubwa duniani kutokana na malighafi inayopatikana.

Aidha, nchi hiyo ina mikataba ya biashara 21 na nchi 28 duniani na tamko hilo linalenga la kuanza mazungumzo ya kuingia mkataba ambao ndani yake una fursa nyingi kwa Watanzania ikiwamo bidhaa za nchi kwenda moja kwa moja Korea.

Rais Samia amehitimisha ziara rasmi ya siku mbili na anatarajia kuanza ziara ya kikazi kwa kuhudhuria mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali kati ya Korea na Afrika, ambako atatoa maoni katika jopo la Kuimarisha Usalama na Chakula na Madini.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini hapa, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, alisema kiongozi huyo kupata nafasi kutoa maoni yake kwenye mkutano huo ni jambo kubwa linalotokana na kazi nzuri iliyofanyika kwenye mtandao wa barabara na kuunganisha reli unaoifanya Tanzania kuwa bora zaidi.

Katika ziara hiyo, Rais Samia anatarajiwa kutunukiwa Shahada ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa (Doctorate Honoris Causal) na Chuo Kikuu cha Anga Korea (KAU) kwa kutambua mchango wake katika mabadiliko ya sera na uongozi wa kimkakati.

Tayari kiongozi huyo ana shahada tano za heshima baada ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu Zanzibar (SUZA), Chuo Kikuu cha Jawaharial Nehru cha India na Chuo Kikuu cha Ankara, Uturuki, wote wakitambua mchango wake kwenye nyanja mbalimbali.

HABARI KITAIFA

FRED LOWASSA:

# Nchimbi usiruhusu ya baba yajirudie

**Na Romana Mallya, MONDULI**

MBUNGE wa Monduli, Fred Lowassa, ameibua tena suala la kukatwa kwa jina la baba yake, Edward Lowassa, Waziri Mkuu wa zamani, katika mchakato wa kupata mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) mwaka 2015.

Safari hii Fred amepongeza msimamo uliooneshwa na Katibu Mkuu wa sasa wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, ambaye alitamka wazi kutokukubaliana na uamuzi uliofanywa wakati huo dhidi ya Lowassa.

Akizungumza jana katika mkutano wa hadhara uliofanyika Makuyuni, wilayani Monduli, mkoani Arusha, Fred alisema kuwa Balozi Dk. Nchimbi alimtendea haki baba yake, Hayati Lowassa.

Mbunge huyo alisema hataona aibu kusema hilo na kama atakuwa amekosea basi asamehewe, akisisitiza kuwa Katibu Mkuu wao wa sasa Balozi Dk. Nchimbi anapaswa kuhakikisha kanuni hazivunjwi tena ndani ya chama chao.

"Siku ile ulitoka katika kikao cha Kamati Kuu kwa heshima, ukasema 'kwa kuwa kanuni za chama zimekanyangwa sitavumilia'. Wewe sasa ni Katibu Mkuu, ukasimamie (kanuni) zisikanyagwe tena," Fred alisema.

Makada 38 walijotosa kuwania kuteuliwa kupeperusha bendera ya CCM katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Hata hivyo, majina ya makada 33, akiwamo Lowassa, yalikatwa katika hatua ya awali. Yalibaki majina matano ya Bernard Membe, Dk. Asha Rose Migiro, January Makamba, Amina Salum Ali na Dk. John Magufuli, ambaye mwishowe alipitishwa kuwa mgombea wa chama hicho, Rais Samia Suluhu Hassan akiwa mgombea mwenza.

Hatua ya kukata jina la Lowassa aliyekuwa anapewa nafasi kubwa, haikufurahiwa na baadhi ya wajumbe wa vikao vya juu vya CCM.

Dk. Nchimbi alikuwa miongoni mwa wajumbe watatu wa Kamati Kuu ya CCM walioitisha mkutano na waandishi wa habari na kueleza kuwa wanapinga uamuzi huo kwa madai kikao kilichofanya uamuzi huo hakikifuata kanuni kwa kuwa majina machache yaliwasilishwa na hayakuhusisha mgombea anayekubalika.

Wajumbe wengine walioungana na Dk. Nchimbi kupinga uamuzi huo ni aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dodoma, Adam Kimbisa na Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Sophia Simba.

Hata hivyo, Dk. Nchimbi na Sophia baadaye waliingizwa katika timu ya kampeni za ushindi wa Dk. Magufuli aliyepitishwa na Mkutano Mkuu wa CCM kuwa mgombea wao wa urais.

Baada ya jina lake kukatwa CCM, Lowassa alijiunga na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) alikoteuliwa kuwa mgombea urais, akiungwa mkono na vyama vingine vya upinzani vilivyounda Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA).

Huko aliipa ushindani mkali CCM, akitangazwa kushika nafasi ya pili katika mbio za urais nyuma ya Dk. Magufuli huku akisaidia vyama vya upinzani kuwa na wabunge wengi katika Bunge la Tanzania. Katika mkutano wa hadhara jimboni Monduli jana, Balozi Dk. Nchimbi, pasi na kujibu chochote kilichotokea mwaka 2015 kwa Lowassa, alisema, "wakulima waheshimu wafugaji, vivyohivyo kwa wafugaji. Tunategemeana unakula ugali na nyama. Ukiona mkulima anamdharau mfugaji, hajui wajibu wake, vivyohivyo kwa mfugaji."

Aliwashukuru wananchi kwa kujali polisi, walimu na manesi kwa kuwa ni kundi ambalo linahangaika usiku na mchana, hivyo changamoto za nyumba walizoeleza ni suala muhimu la kufanyiwa kazi.

Balozi Nchimbi alisema mwezi mmoja na nusu mbunge wa jimbo hilo alimtafuta, akaomba asaidiwe kusukuma suala la miradi miwili mikubwa ya maji inayotakiwa kutekelezwa na alimtafuta waziri mwenye dhamana na kumtaka aende kulishughulikia. Tayari mkataba umetiwa saini.

Alimpigia simu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, naye aliwaeleza wananchi kuwa mahitaji ya maji ni zaidi ya lita 300,000 jimboni humo na uwezo uliopo ni zaidi ya lita 100,000.

Alisema serikali imeshaagiza kujengwe mradi wa Sh. bilioni saba na tayari mradi umeshatiwa saini na mkandarasi anatafuta mabomba. Yeye (Aweso) atasimamia ukamilike kwa wakati.

Kuhusu kumalizia jengo la kulaza wagonjwa katika Hospitali ya Makuyuni, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, akizungumza kwa njia ya simu, aliahidi watafika kwa ajili ya tathmini na kuhakikisha jengo hilo linajengwa na kuhudumia wananchi wa Monduli.

Balozi Dk. Nchimbi alisema kuwa kiongozi asiyeguswa na kero za wananchi hatoshi katika nafasi yake.

"Wananchi wote mliokuja kushirikiana nasi hapa, tunawashukuru sana, niwahakikishe CCM imeendelea kusimamia serikali zake kuona zinahudumia wananchi kwa upendo," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, alisema kuna changamoto ya ajira kwa vijana, ndio maana wanagusa sekta ya utalii ambayo sasa ina watalii wengi. Alisema yuko tayari kupokea maagizo yoyote halali ya chama na kuyatekeleza.

Katika mkutano huo, Balozi Nchimbi pia aliahidi kukabidhi pikipiki moja leo kwa mama aliyeomba msaada huo na Mkuu wa Mkoa huo. Makonda naye akaahidi kutoa pikipiki kwa kijana mwingine.

Akiwa mkoani Manyara juzi, Balozi Dk. Nchimbi alisema anavutiwa na aina ya wakuu wa mikoa ambao wanaposikia matatizo ya wananchi wanakwenda kuyatatua na si wakuu wa mikoa mabwana wakubwa ambao muda wote wanatamani kujionesha wao ni kina nani.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

TANGAZO



KILIMANJARO
DRINKING WATER
A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
Mshindi wa
SUPERBRANDS
AFRIKA MASHARIKI
2022-2024
VOTED
Superbrands
EAST AFRICA'S CHOICE
2022-2024
Asanteni wateja wetu
Hii ni yetu sote
kilimanjaro_drinking_water
kilimanjarodrinkingwater
kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422

# Serikali yasifu wanawake, vijana kuwezesha bilioni 10/- za mtaji

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imepongeza programu ya kutoa mafunzo ya ujasiariamali, elimu ya fedha na mitaji wezeshi zaidi ya Sh. bilioni 10 kwa vijana na wanawake wajasiriamali nchini.

Mkurugenzi wa Jinsia wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Badru Abdunuru alitoa pongezi hizo kwa Taasisi ya CRDB Bank Foundation wakati wa hafla ya mafunzo ya ujasiriamali na elimu ya fedha pamoja na kukabidhi mitaji wezeshi ya jumla ya Sh. milioni 150 kwa wanachama wa Asasi ya Data Sustainable Development ya Dar es Salaam, jijini mwishoni mwa wiki.

Katika mafunzo hayo ilibainishwa kuwa kati ya Sh. bilioni 10 za mtaji wezeshi zilizotolewa mpaka sasa, wakazi wa Dar es Salaam wamepokea zaidi ya Sh. bilioni 3.6.

Abdunuru alisema ni dhahiri kuwa wanawake na vijana ndio injini ya uchumi kwa kuwa wana uwezo mkubwa wa kuliinua taifa kiuchumi. Kwa kuzingatia Ripoti ya Sensa na Makazi ya mwaka 2022, alisema asilimia 51 ya watu wote nchini ni wanawake na asilimia 75 ni vijana, hali inayodhihirisha umuhimu wa kundi hilo kwa nguvukazi ya taifa.

"Hata hivyo, wanawake na vijana wanakabiliwa na changamoto nyingi zikiwamo mila na desturi kandamizi, elimu duni, ukosefu wa mitaji na stadi za ujasiriamali. Tukizitambua changamoto hizi, serikali imechukua hatua mbalimbali zinazolenga kujenga uchumi jumuishi na shirikishi ili kuwakomboa kiuchumi.

"Tunaendelea kufanya kazi kwa bidii kufikia malengo ya Jukwaa la Kimataifa ya Kukuza Usawa wa Kijinsia hususan katika haki na usawa wa kiuchumi. Ninaipongeza taasisi hii kwa kuja na ubunifu huu unaounga mkono jitihada za serikali kukomboa kiuchumi vijana na wanawake," alisema. Ili kuwezesha zaidi wajasiriamali wanawake na vijana, mkurugenzi huyo alisema ni muhimu kwa wadau wote wa maendeleo kushiriki mkakati huo kwa kuwa serikali pekee haitoweza kutatua changamoto zote zilizopo.

"Niipongeze taasisi hii kwa kuja na programu hii ambayo inalenga kuboresha maisha na kuimarisha biashara za vijana na wanawake kwa kuwapa mafunzo na ushauri wa namna bora ya kusimamia na kuendesha biashara zao, pamoja na kuwapa mitaji wezeshi.

"Ninaamini mmefungua milango kwa taasisi nyingine kubuni namna zinavyoweza kuyashirikisha makundi haya katika mipango yao," alisema Abdunuru.

Akizungumza kwenye mafunzo hayo, Mkurugenzi wa taasisi inayoratibu programu hiyo, Tully Mwambapa alisema mpaka mwishoni mwa Mei wameshatoa mafunzo kwa zaidi ya wanawake na vijana 400,000 ambao baadhi yao wamenufaika na mitaji wezeshi yenye thamani ya Sh. bilioni 10.

Mafanikio hayo, Tully alisema yasingeweza kufikiwa bila kushirikisha wabia wao wa kimkakati kama ilivyo Asasi ya Data Sustainable Development yenye zaidi ya wanachama 1,800 na wengine wengi kuanzia mashirika ya kimataifa, taasisi za serikali na vikundi vya wanawake wajasiriamali.

# Saruji Mbeya yatoa gawio bil. 3/- kwa serikali

**Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Saruji ya Mbeya inayojulikana kwa chapa yake ya Tembo ambayo pia ni kampuni tanzu ya Amsons, imetoa gawio la Shilingi bilioni tatu kwa serikali. Mafanikio hayo ni matokeo ya mabadiliko yaliyofanywa na wanahisa hususan Serikali ya Awamu ya Sita baada ya kutengeneza mazingira mazuri na rafiki kwa wawekezaji kupitia falsafa yake ya nguzo nne za R (4Rs).

"Tunajivunia mafanikio haya kwasababu kwa kipindi cha miaka 10 kampuni hii haikuwahi kutoa gawio kwa wanahisa wake, mara ya mwisho kufanya hivyo ilikuwa mwaka 2014 haya ni mabadiliko ya kungwa mkono," alisema Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu wakati wa kikao kifupi cha wanahisa na menejimenti kilichofanyika jana kiwandani hapo. Alisema kampuni hiyo pia inajivunia kuwa ya kwanza kumilikiwa na kuendeshwa na wazawa ikiwa ni uwezeshaji uliofanywa na serikali.

Serikali kama mmoja wa wanahisa katika kampuni hiyo ikiwa na umiliki wa asilimia 25 na kupitia kwa Msajili wa Hazina, imepokea Shilingi bilioni tatu na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) wenye hisa asilimia 10 imepokea Sh. bilioni 1.2 kama gawio.

Mchechu alisema, umiliki wa hisa nyingi za asilimia 65 ndani ya kampuni ya Saruji Mbeya, zilichukuliwa na kampuni za Amsons ya Tanzania kutoka kwa Holcim ya Uswisi.

Wanahisa walitembelea kiwanda cha kuzalisha saruji cha Mbeya, Mei 31, 2024 na walisisitiza kuendelea kuunga mkono na kuhakikisha kuna ukuaji endelevu kwa miaka ijayo kwa faida ya wadau wote na kuongeza thamani kwa wanahisa wake.

Akizungumza na wafanyakazi kiwandani hapo, Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu alisema uwapo wa kiwanda hicho ni maono ya Mwalimu Nyerere miaka ya 1978 ambayo yanapaswa kulindwa kwa manufaa ya vizazi vya Tanzania, na ili kufanya vizuri zaidi kunahitaji kupunguza gharama za uzalishaji ili kukuza faida.

Mbeya Cement Company Limited (MCCL) ilianzishwa nchini Tanzania chini ya Sheria ya Makampuni, 2002 kama kampuni binafsi iliyoko Songwe, Mbeya ambayo inajishughulisha na utengenezaji na uuzaji wa saruji.



Baadhi ya wakazi wa Mbezi Msumi jijini Dar es Salaam wakiwa wameegesha magari yao karibu na sehemu ya daraja la Kwa Ndee linalounganisha Madale Mwisho na Msumi ambalo lilibomoka kwa miezi saba sasa bila hatua zozote za kurejesha katika hali yake ya zamani ili liweze kutumiwa na wakazi hao. **PICHA: MWANDISHI WETU**

# Bunduki 91 na risasi 276 zanaswa mapori ya TAWA

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BUNDUKI 91, risasi 276 na watuhumiwa 2,304 wamekamatwa katika mapori yanayosimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA).

Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki alipowasilisha bungeni jijini hapa makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema kuwa katika kudhibiti ujangili na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa, mamlaka hiyo imeendelea kuimarisha ulinzi wa rasilimali za wanyamapori kwa kufanya doria mbalimbali na kutumia vikosi vya mwitikio wa haraka.

Waziri Angellah alisema kuwa hadi kufikia Aprili 2024, doria 11,593 sawa na asilimia 80 ya lengo la doria 14,487 zilikuwa zimefanyika.

"Kupitia doria hizo, jumla ya mifugo 41,294, watuhumiwa 2,304, bunduki 91 na risasi 276 zimekamatwa pamoja na kutegua mitego 2,056 ya nyaya za kutegea wanyamapori.

"Kufuatia kuimarika kwa ulinzi katika maeneo yanayosimamiwa na mamlaka, idadi ya vifo vya tembo wanaouawa kwa ujangili imepungua kutoka tembo sita mwaka wa fedha 2022/23 hadi tembo watatu Aprili 2024," alisema.

Waziri Angellah alisema TAWA pia imekarabati kilomita 764.5 za barabara za doria katika Mapori ya Akiba Kizigo na Selous na ujenzi wa chumba maalum cha ufuatiliaji faru katika Pori la Akiba Maswa.

Alisema mamlaka pia imenunua pikipiki 10 kwa ajili ya kuimarisha shughuli za uhifadhi pamoja na kuwapatia mafunzo ya kijeshi ya ukakamavu na utayari askari wa wanyamapori 458.

Alisema TAWA pia imeendelea kushiriki maonesho na matukio mbalimbali kwa lengo la kutangaza vivutio vya utalii na fursa za uwekezaji katika maeneo yake. Miongoni mwa maonesho hayo ni Abu Dhabi International Hunting & Equestrian Exhibition (ADIHEX, 2023), Dallas Safari Club International - USA na maonesho ya ndani ya nchi.

"Kufuatia juhudi hizo, idadi ya watalii wa picha waliotembelea maeneo yanayosimamiwa na mamlaka imeongezeka kutoka watalii 139,749 Aprili 2023 hadi kufikia 157,725 Aprili 2024.

"Mamlaka imeendelea kukusanya mapato yatokanayo na shughuli za utalii ambapo hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya Sh. bilioni 57.647 sawa na asilimia 73.54 ya lengo la mwaka zimekusanywa," alisema.

NCAA.

Kuhusu Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), Waziri Angellah, alisema kuwa katika kuimarisha ulinzi wa rasilimali za wanyamapori, mamlaka hiyo imefanya doria 251 zilizowezesha kukamatwa watuhumiwa 339 wa makosa mbalimbali, mifugo 16,683, silaha moja - Riffle, magazine 4, meno ya tembo 28 na vipande 67 pamoja na kutegua mitego 23 ya nyaya za kutegea wanyamapori.

Alisema NCAA pia imesafisha mipaka yenye jumla ya kilomita 116 na kuweka vigingi 26 kwa ajili ya kuepusha migogoro ya mipaka na matukio ya moto.

"Wizara kwa kushirikiana na Jeshi la Wananchi (JWTZ) imeboresha kilipuzi (bomu baridi) kwa ajili ya kudhibiti tembo wanapoingia kwenye maeneo ya wananchi. Bomu hilo lilizinduliwa rasmi tarehe 13 Mei, 2024 na baada ya uzinduzi tarehe 22 Mei 2024 wizara ilikabidhiwa rasmi mabomu baridi 4,000 katika Makao Makuu ya Shirika la Mzinga-Morogoro kwa ajili ya kuanza kutumika kwenye halmashauri 20 zilizo katika mifumo ikolojia mitano nchini," alisema.

Halmashauri hizo ni Nachingwea, Liwale, Manispaa ya Lindi (Mchinga), Mtama, Ruangwa, Tunduru, Namtumbo, Karatu, Same, Mwanga, Mvomero, Mkinga, Korogwe, Meatu, Busega, Itilima, Bariadi, Bunda Mjini, Bunda Vijijini na Karagwe.

Udhibiti wa matukio ya moto na wanyamapori wakali na waharibifu ni utekelezaji wa hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) iliyomo katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2021/22.

Katika ripoti hiyo, CAG anapendekeza serikali ije na mikakati ya kukabiliana na matukio ya moto katika hifadhi za taifa na kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu ambao wamekuwa wakisababisha vifo kwa wakazi wa maeneo wanakovamia, pia uharibifu wa mali, hasa mazao.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunahitaji wawakilishi imara mashindano ya Kagame Cup

**MASHINDANO** ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati maarufu Kombe la Kagame yametangazwa kurejea tena mwaka huu.

Taarifa rasmi iliyotolewa hivi karibuni na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), likisema mashindano hayo yatafanyika kuanzia Julai 20 hadi Agosti 4, mwaka huu huko Visiwani Zanzibar.

Mara ya mwisho michuano hiyo ilifanyika mwaka, 2021 na Express kutoka Uganda ilitwaa ubingwa baada ya kuwafunga bao 1-0 Nyasa Big Bullets ya Malawi (timu iliyoalikwa), katika mechi ya fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

CECAFA imesema nchi zote 12 wanachama wa baraza hilo ambazo ni Tanzania Bara, Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda, Ethiopia, Somalia, Sudan, Sudan Kusini, Djibouti, Eritrea na wenyeji Zanzibar wamethibitisha kushiriki katika mashindano hayo.

Bingwa wa msimu husika hupata tiketi ya kushiriki mashindano hayo na CECAFA imesema kurejea kwa michuano hiyo kutawasaidia wawakilishi wake kujiandaa na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika.

Hata hivyo, hadi mashindano hayo ambayo bado yamebeba jina la Rais wa Rwanda, Paul Kagame, kutokana na ufadhili wake mbalimbali anaotoa ikiwamo fedha za zawadi kwa washindi (Dola za Marekani 60,000), yalipoteza nguvu baada ya klabu kugomea kushiriki kwa sababu mbalimbali.

Baadhi ya timu zilisema haziwezi kushiriki mashindano hayo kwa sababu zimewaruhusu wachezaji wake kwenda mapumzikoni kutokana na kalenda ya michuano hiyo kuchelewa kutolewa, lakini klabu nyingine zikidai zimejipanga kuweka kambi ughaibuni kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya.

Sababu zote hizi, zilichangia 'kuua' au kuondoa ladha ya ushindani ambayo ilizoeleka wakati wote wa mashindano haya yalipokuwa yakifanyika na pengine pia yakiwa ni moja ya michuano iliyokuwa inasubiriwa kwa hamu na mashabiki wa soka wa ukanda huu.

Kama ambayo CECAFA imekuwa ikifanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya wasichana na wanawake, timu zake kufuzu fainali za Kombe la Dunia ikiwamo Serengeti Girls ya Tanzania iliyofuzu michuano ya U-17 mwaka juzi, Twiga Stars imekata tiketi ya kucheza Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (WAFCON), lakini pia timu moja kati ya Kenya na Burundi, itafuzu kushiriki fainali zijazo za mashindano hayo, yote yanatokana na kuwapo kwa michuano mbalimbali ya vijana kwa wasichana.

Umefika wakati kwa kila mwanachama wa CECAFA kuhakikisha timu yake iliyofuzu kushiriki mashindano hayo inaleta kikosi cha kwanza ambacho kitaonyesha kiwango bora na kufikia malengo yaliyotarajiwa ya kucheza soka la ushindani.

Hatutarajii kuona mashindano haya yamerejea na nchi washiriki wanayapuuzia, tunawakumbusha viongozi wa klabu kuipa umuhimu unaostahili michuano hii ambayo pia ni daraja lingine la kuwatangaza wachezaji, makawala wa timu za Ulaya wanaosaka vipaji Afrika hutuma wawakilishi wao kwa ajili ya kutafuta nyota wenye vipaji.


Katika dunia ya sasa ambayo hata kama mawakala hawajakanyaga ardhi ya Tanzania, wanaweza kufuatilia michuano hii kokote waliko duniani, tunawakumbusha wachezaji watakaopata nafasi ya kucheza, kujituma na kucheza kwa bidii kwa ajili ya kutimiza ndoto zao za kusajiliwa na timu kutoka mataifa yaliyoendelea.

Wachezaji wanatakiwa kufahamu kupitia mashindano ya Kombe la Kagame, wachezaji mbalimbali wamepata ofa za kujiunga na timu za Ulaya na sasa ni nyota wakubwa wanaotegemewa katika mataifa waliyozaliwa, lakini wakipokea mishahara minono inayosaidia kuendesha maisha yao binafsi pamoja na familia.

TFF na vyama vingine, si vibaya kukutana na wawakilishi kwa lengo la kujipanga kuelekea mashindano hayo na kwa wenyeji, Tanzania Bara na Zanzibar, si vyema kombe hili likabebwa na wageni wakati uwezo wa kulibakisha upo endapo kila upande utayapa umuhimu unaostahili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Wachezaji tumieni mapumziko vizuri, acheni kuzidisha starehe

**MSIMU** wa mashindano ya ndani na nje ya nchi umemalizika rasmi jana, baada ya kufanyika kwa fainali ya mashindano ya Kombe la FA.

Hii ni baada ya kumalizika kwa Ligi Kuu Tanzania Bara Jumanne iliyopita, ambapo baada ya hapo wachezaji wa timu nyingine, isipokuwa Yanga na Azam FC, ambao jana walicheza fainali, walirejea majumbani kwao kwa ajili ya kupumzika na kujiandaa kwa msimu mpya wa mashindano.

Wachezaji hao wanatoka katika mikoa mbalimbali hapa nchini huku wale wanaotoka nje ya nchi, pia kila mmoja anarejea kwao kuungana na familia zao baada ya kumaliza majukumu.

Ni kipindi ambacho wachezaji wanakwenda kupumzisha miili na akili baada ya mikiki ya msimu mzima, ya uwanjani, pamoja na kusafiri huku na huko kwa kutumia ndege au magari. Kusema kweli inachosha sana kwa sababu hata msafiri tu wa kawaida ambaye hachezi mpira, akishafika anakuwa na uchovu unaochukua siku nzima kurejea katika hali ya kawaida.

Sasa pata picha kwa mchezaji ambaye amesafiri kwa umbali mrefu, anatakiwa kesho yake acheze soka, halafu asafiri tena akacheze katika mkoa mwingine siku chache tu baadaye.

Niwape pongezi wachezaji wote walioshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kazi kubwa ambayo wameifanya, licha ya hiyo ni kazi yao, lakini wanaifanya katika mazingira magumu, ikizingatia miundombinu ya nchi yetu kuanzia usafiri na hata baadhi ya viwanja kutokuwa rafiki kama wenzetu huko Ulaya.

Ushauri wangu ni baada ya kazi kubwa walioifanya, ikiwamo kutoa burudani kwa mashabiki, wanapaswa wapumzike kweli katika kipindi hiki.

Nikisema wapumzike kweli inamaanisha nyota hao wanatakiwa kutumia muda zaidi wakiwa na familia zao ambazo waliziacha peke yao kwa muda mrefu.

Haikatazwi kujiliwaza na kufanya starehe, au burudani, kwani hata wachezaji huko nje tunawaona 'wakila bata' baada ya msimu kumalizika, lakini wasijisahau sana wakafanya hivyo kupitiliza.

Kuna wachezaji kipindi hiki sasa ndiyo wanapata nafasi ya kushinda baa, kuzurura huko na huko na kufanya mambo mengi ambayo badala ya kupumzisha, wanauchosha mwili.

Wenzao wa Ulaya wanafanya hivyo kwa kiasi tu, lakini baada ya hapo wanafanya mazoezi madogo madogo, na kupumzika, ili kuurudisha mwili kwenye nguvu tayari kwa ajili ya kurejea kuanza msimu mpya.

Starehe za kupitiliza hufanya wachezaji wanaporejea kuwa na vitambi au uzito mkubwa, hivyo kuwafanya makocha wawe na kazi kubwa ya 'kuwakamua' kwa mazoezi makali.

Vile vile starehe za kizembe, hufanya mwili kuwa dhaifu, na kuathiri hata kiwango cha mchezaji husika mwanzoni mwa msimu.

Licha ya kupumzika, kuburudika au kwenda kwenye matembezi kama mbuga za wanyama, na sehemu mbalimbali za vivutio kwa ajili ya kupumzisha akili, wachezaji wanatakiwa kujua kuwa soka ni ajira yao, hivyo angalau wiki moja kabla ya kuanza 'pre season', wanatakiwa kujiweka fiti, ili wanaporejea wawe katika 'shepu' nzuri ya kimichezo, ambayo haitowafanya kuanza vibaya mechi za mwanzo.

Tumeona huko nyuma baadhi ya wachezaji wakianza vibaya mechi za mwanzo, hadi baada ya michezo kadhaa ndipo wakarejea katika viwango vyao kutokana na kushindwa kujitunza wakati huu wa mapumziko.

Huu si utamaduni mzuri, wachezaji wanatakiwa kufuata maadili ya soka kwa ajili ya kufanya wajibu katika klabu zao ambazo zinawalipa fedha nyingi, lakini pia mustakabali wa maisha yao ya soka, kwa sababu huenda wakafanya kazi hiyo katika muda mfupi.

# Wanunua mashine kuzalisha tani 30 za mchele kwa siku

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

CHAMA cha Ushirika wa Wakulima wa Umwagiliaji Ruvu (CHAURU) kimenunua mashine ya kisasa ya ukoboaji mpunga yenye uwezo wa kuzalisha tani 30 za mchele kwa siku sambamba na kununua pampu nne za umwagiliaji.

Mwishoni mwa wiki aliyekuwa Mwenyekiti wa chama hicho, Sadala Chacha, alibainisha hayo alipotoa taarifa kwenye Mkutano Mkuu Maalum wa uchaguzi wa chama hicho uliofanyika Ruvu.

Sadala alisema ununuzi wa mashine hiyo ni moja ya mafanikio yaliyopatikana wakati wa uongozi wa bodi iliyomaliza muda wake, wakifanikiwa pia kupunguza uchakavu wa miundombinu ya umwagiliaji kwa kujenga upya mifereji mikuu.

Pia alisema kuwa kwa misimu mitatu mfululizo uzalishaji umeongezeka kutoka tani 4.5 hadi 6.5 huku hisa zikiongezeka kutoka 300,000 wakati bodi hiyo inaingia madarakani hadi kufikia milioni 86.

Pamoja na mafanikio hayo, Sadala alisema chama hicho pia kimeainisha vikwazo wanavyokabiliana navyo kuwa ni pamoja na uchakavu wa miundombinu ya umwagiliaji kwa asilimia 60 kutoka asilimia 80 iliyokuwapo wakati wanakabishiwa shamba hilo mwaka 2004.

Sadala alitaja kikwazo kingine ni ukosefu wa fedha za kutekeleza mpango wa upakuzi wa skimu mpya ya umwagiliaji mpunga yenye ukubwa wa hekta 1,380 pamoja na baadhi ya wafugaji kulisha mifugo yao kwenye skimu na kusababisha uharibifu wa miundombinu.

Katika mkutano huo wanachama walichagua wajumbe wa bodi; mwenyekiti pamoja na wajumbe wa Kamati ya Maadili na Usuluhishi.

Kabla ya uchaguzi huo, Ofisa Ushirika, Rafael Kajale ambaye alikuwa msimamizi wa uchaguzi huo, alisema waliioomba nafasi ya ujumbe wa bodi walikuwa 34 na baada ya usaili walibaki wanane kati ya watano wanaotakiwa na baadaye mmoja alitolewa kutokana na utata uliotokana na kuwa kiongozi wa chama cha siasa.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akitazama nguo za batiki alipotembelea banda la maonesho la wanawake wajasiriamali waliowezeshwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi baada ya kuzindua kituo cha baraza hilo kilichoko Karumwa wilayani Nyang'wale Mkoa wa Geita jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# ACT: Kinachojiri 'Sauzi' funzo kwa CCM

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema yanayoendelea katika Uchaguzi Mkuu wa Afrika Kusini yanafaa kuwa somo kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu, alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki, baada ya chama tawala Afrika Kusini, ANC kushindwa kupata kura za kuunda serikali peke yake. Alisema ipo siku CCM itajikuta katika mazingira hayo.

Shaibu alikuwa anazungumza na viongozi wa chama hicho wa mkoani Pwani wakati wa kikao kilichofanyika Kata ya Mwandege, Jimbo la Mkuranga juzi.

"Kinachotokea kwa ANC kule Afrika ya Kusini kinapaswa kuwa funzo kwa CCM kuwa ukipuuza hisia za wananchi, nao watazungumza kupitia sanduku la kura," alisema Shaibu.

Alisema kuwa kwa mara ya kwanza tangu kushika serikali mwaka 1994, ANC imeshindwa kufikisha asilimia 50 ya kura ili kuunda serikali, uchambuzi ukionesha ni ishara na matokeo ya ANC kushindwa kuwajibika kwenye masuala muhimu ya wananchi. Katibu huyo alitaja baadhi ya masuala hayo kuwa ni ukosefu wa ajira, huduma mbovu ya umeme, ufisadi na utawala mbovu.

"Ni dhahiri kuwa hata nchini kwetu, ninaamini siku za CCM kutawala nazo zinahesabika kwa sababu kama ilivyo kwa ANC, Chama Cha Mapinduzi nacho kimepuuza kwa kiasi kikubwa hisia za Watanzania," alidai.

Shaibu alisema, "Uchambuzi wetu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) unaonesha kuwa fedha za umma Sh. trilioni 3.14 zimepotea katika mazingira ya ubadhirifu na hakuna hatua yoyote ya maana iliyochukuliwa dhidi ya ubadhirifu huo."

Katibu Mkuu Shaibu pia alisema ACT Wazalendo inawasiliana na asasi mbalimbali za kiraia kufungua kesi mahakamani ili uchaguzi ujao wa serikali za mitaa usimamiwe na Tume Huru ya Uchaguzi badala ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

# Raia Canada kizimbani shtaka la udanganyifu bil. 2/- za Patel

**Na Grace Gurisha**

MFANYABIASHARA Stefan Nagy, raia wa Canada amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, akikabiliwa na shtaka la kujipatia zaidi ya Sh. bilioni mbili kwa njia ya udanganyifu kutoka kwa Mitul Patel kwa madai angempelekea kilo 15 za madini aina ya dhahabu.

Nagy (55) alipandishwa kizimbani katika mahakama hiyo mwishoni mwa wiki mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Franco Kiswaga.

Aliposomewa shtaka linalomkabili, alishindwa kutimiza masharti ya dhamana, hivyo kupelekwa mahabusu.

Akimsomea hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Mwandamizi Grace Mwanga alidai mshtakiwa alitenda kosa hilo Februari 5, mwaka huu katika Benki ya India Tanzania Limited, Mtaa wa Ohiyona Sokoine, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam.

Alidai mshtakiwa akiwa eneo hilo alijipatia Sh. 2,074,373,229 kutoka kwa Mitul Bharat Kumar Patel kwa madai kwamba angempelekea kilo 15 za madini aina ya dhahabu.


Baada ya kusomewa shtaka hilo, mshtakiwa alikana kutenda kosa hilo. Upande wa Mashtaka ulidai haujakamilisha upelelezi na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa kwa kesi hiyo.

Hakimu Kiswaga alimweleza mshtakiwa kuwa ili awe nje kwa dhamana, anatakiwa awe na kuwasilisha mahakamani fedha taslimu au hati ya mali zisizohamishika zenye thamani ya nusu ya kiwango kilichohusishwa katika shtaka hilo.

Kwa kuwa mshtakiwa si raia wa Tanzania, hakimu alisema anatakiwa kuwasilisha hati yake ya kusafiria mahakamani, akitaka kusafiri nje ya nchi aombe rukhsa mahakamani na awe na wadhamini wawili.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed





Mchungaji Abraham (katikati), akikabidhi tuzo kwa Ofisa Masoko wa Taasisi ya Watumishi Housing Investments (WHI), David Mwaipaja (kushoto) na Ofisa Uwekezaji, Fidelis Lyimo, baada ya taasisi hiyo, kuibuka mshindi katika kipengele cha kampuni bora ya mwaka 2024 katika usimamizi wa mifuko ya uwekezaji, wakati wa hafla ya utoaji tuzo iliyoandaliwa na Taasisi ya The Global CEO kwa kushirikiana na Africa Company of the Year Award (ACOYA), jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mawaziri EAC wakubaliana kuondoa vikwazo biashara

**Na Joseph Mwendapole**

MAWAZIRI wanaosimamia sekta ya Biashara, Viwanda, Fedha na Uwekezaji katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), wamekubaliana kuendelea kuboresha mazingira ya biashara katika jumuiya hiyo kwa kuanza na kuondoa vikwazo visivyo vya kikodi.

Wamekubaliana pia kurahisisha uvushaji wa mizigo mipakani na kuimarisha utendaji wa miundombinu ya kusaidia biashara ikiwamo vituo vya kutoa Huduma Pamoja Mpakani (OSBP).

Vilevile, wamekubaliana mapendekezo ya viwango mbalimbali vya ushuru wa forodha vitakavyotumika katika mwaka wa fedha 2024/25 ambavyo vitachochea ukuaji wa uchumi wa nchi wanachama.

Makubaliano hayo yalifikiwa mwishoni mwa wiki kwenye Mkutano wa 44 wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Biashara, Viwanda, Fedha na Uwekezaji (SCTIFI) la Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika katika Makao Makuu ya Jumuiya hiyo jijini Arusha.

Akizungumzia makubaliano hayo, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema hatua hiyo imefikiwa ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa na Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kuwataka watendaji na viongozi waliopo chini yao kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na kuondoa vikwazo vya kibiashara katika jumuiya.

Waziri Nchemba alitaja maeneo yaliyofanyiwa maboresho katika mkutano huo kuwa ni pamoja makubaliano kuhusu viwango vya tozo za barabara kwa nchi wanachama kutoka Dola za Marekani 16 hadi 10.

Alitaja eneo lingine kuwa ni makubaliano ya utekelezaji wa mkakati wa Himaya Moja ya Forodha hasa kwa upande wa Tanzania na Kenya na Tanzania ilishaanza utelezaji wake.

Alisema Kenya imeahidi kuanza kupitisha bidhaa za Tanzania katika mfumo wa himaya moja ya forodha mara moja na kufikia mwenzi Julai 2024 na kuleta wafanyakazi wake wa mamlaka ya forodha kwa ajili ya kuwezesha ukaguzi kabla mzigo haujaanza kuondoka ili usisimame mpakani.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuondoa msongamano, usumbufu na upotevu wa mapato kwa serikali na wasafirishaji wa bidhaa kati ya Tanzania na Kenya.

"Tanzania tumekuwa tukikabiliwa na tatizo la msongamano wa malori katika mipaka yetu ikiwamo Namanga, Sirari, Holili na Hororo, hii imechangiwa na kutokuwapo kwa maofisa wa KRA upande wa Tanzania ambao wangesaidia kufanyia kazi nyaraka za kupitisha mzigo mpakani kabla gari husika halijafika mpakani tofauti na ilivyo sasa, utekelezaji wa ahadi hii utasaidia kutatua tatizo hili lililo tusumbua kwa muda mrefu," alisema Dk. Nchemba.

Katika hatua nyingine, Waziri Nchemba aliwaongoza mawaziri wenzake kuzindua mfumo mpya wa kielektroniki wa masuala ya forodha unaolenga kuongeza ufanisi katika biashara kwa kuweka mazingira ya uwazi, uwajibikaji na hatimaye kuongeza mapato kwa serikali za nchi wanachama wa Jumuiya. Mkutano huo wa mawaziri ulitanguliwa na wa ngazi ya wataalamu uliofanyika Mei 27 hadi 29, 2024 na ngazi ya Makatibu Wakuu uliofanyika Mei 30, 2024.

Ujumbe wa Tanzania katika mkutano huo ni pamoja na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba ambaye aliongoza ujumbe wa Tanzania, Shariff Ali Shariff, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais anayeshughulikia Kazi, Uchumi na Uwekezaji-Zanzibar, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki, Stephen Byabato na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe.






## Waomba nishati mbadala kuhifadhi misitu Udzungwa

**Na Jenifer Gilla**

WAKAZI wa vijiji vinavyopakana na Hifadhi ya Milima ya Udzungwa wameomba serikali kwa kushirikiana na wadau wawapelekee nishati mbadala ya kupikia ili waepuke matumizi ya kuni na mkaa yanayochochea kukata miti kwenye hifadhi.

Kauli hiyo imetokana na elimu ya umuhimu wa uhifadhi wa misitu wanayopewa na wadau wa uhifadhi kwa ufadhili wa USAID, Tuhifadhi Maliasili.

Mkazi wa Kijiji cha Kiberege, Salma Selemani, alisema baada ya kupatiwa elimu ya utunzaji misitu na Taasisi ya Asscioazione Mazingira wameona kuna umuhimu mkubwa wa kutokata miti katika hifadhi hiyo, lakini hawana namna.

Alisema ingawa kuna nishati ya gesi ya kupikia katika eneo hilo, lakini inauzwa bei ya juu ambayo hawezi kuimudu kutokana na kipato chake kuwa kidogo.

"Mimi binafsi natamani mtu yeyote asiingie kukata miti katika msitu ule, lakini sasa tutatumia nini kupikia wakati hakuna njia mbadala ya kupata nisati nyingine ya bei nafuu," alihoji.

Mkazi wa Mang'ula B, Dibana Kawaga alisema, wanashawishika kuingia msituni kufuata kuni kwasababu hawana chanzo kingine cha kupikia kinachopatikana kwa bei nafuu zaidi ya kuni na mkaa.

Aliiomba serikali kwa kushirikiana na wadau wawapelekee gesi yenye gharama nafuu watakayoweza kuimudu ili wapunguze matumizi ya kuni na mkaa ambayo ndio chanzo kikuu cha wao kuingia msituni.

Mkazi wa Kijiji cha Sole, Suna Kolela, alisema pamoja na kupatiwa elimu ya uhifadhi mazingira na kushirikishwa katika shughuli za uhifadhi, lengo la kuilinda milima hiyo haitofanikiwa kama miti itaendelea kukatwa.

Mkazi wa Kijiji cha Mangu'la A, Dalas Msumia, alishauri uongozi wa wilaya hiyo kufanya utaratibu wa kuwafikishia wananchi wa vijiji hivyo nishati mbadala ya bei nafuu ili kumaliza tatizo la uvamizi wa misitu.

Mhifadhi Mkuu, Theodora Aloyce, alisema wanafanya utaratibu wa kutafuta wadau watakaojitolea kuwapelekea majiko ya gesi wanavijiji hao ili kukabiliana na tatizo la uvamizi wa msitu.

Alisema kitendo cha wananchi kuomba kupelekewa nishati mbadala kinaonyesha ni namna gani elimu wanayopewa wanaielewa ingawa tatizo la ukataji miti katika hifadhi hiyo bado ni kubwa.

Alisema bado wanaendelea kushirikiana na wadau wa uhifadhi kutoa elimu kwa jamii, ikiwamo kutumia nishati safi ya kupikia kama gesi na mkaa mbadala kwa utaratibu mzuri ili idumu muda mrefu.

Meneja Uhusiano wa Jamii wa shirika lisilo la kiserikali la Reforest Africa linalotekeleza Mradi wa Urejeshaji Shoroba unaofadhiliwa na USAID Tuhifadhi Maliasili, Peter Paul, alisema kupitia mradi huo wanatoa mafunzo ya kuhifadhi misitu kwa vijiji vinavyozunguka hifadhi hiyo.

Alisema pia wanazalisha miti ya asili na kushirikiana na wanakijiji kupanda katika shoroba ili kuirejesha katika hali yake ya zamani kwa manufaa ya viumbe vinavyoishi katika shoroba hiyo na wananchi pia.

"Kwa mfano kwa sasa tunashirikiana na wanakijiji kupanda miti katika msitu wa Magombera unaounganisha hifadhi za Udzungwa na Nyerere Selous ili kuurejesha katika hadhi yake," alisema.

Alisema malengo ya mradi huo wa miaka miwili unaoisha Juni 2025 ni kupanda miti 100,000 na mpaka kufikia Juni, mwaka huu, watakuwa wameshapanda miti 50,000.

Alisema kwa sasa wanaendelea kuzalisha miti ya asili kwa kuchanganya mbegu za aina mbili inapofika kimo sahihi wanakwenda kuipanda kwenye eneo husika.




Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, akiteta jambo na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Stephen Byabato, kwenye Mkutano wa 44 wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Biashara, Viwanda, Fedha na Uwekezaji (SCTIFI) la Jumuiya ya Afrika Mashariki jijini Arusha. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Waliohama NCAA kwenda Tanga wafikia 8,960

**Na Godfrey Mushi,** NGORONGORO

WAFUGAJI wa jamii ya Kimasai, waliohama kwa hiari ndani ya eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) kwenda kuanza maisha mapya katika maeneo mengine nchini, ikiwamo Msomera mkoani Tanga, wamefikia 8,960.

Idadi hiyo ni sawa na kaya 1,472, huku kanzidata ya NCAA ikionyesha mifugo iliyoondolewa ndani ya hifadhi hiyo hadi sasa ni 38,098.

Kwa mujibu wa Ofisa Uhifadhi Mkuu wa NCAA ambaye ndiye Meneja Mradi huo, Flora Assey, kaya hizo zimehama kwenda Kijiji cha Msomera, Wilaya ya Handeni, Kijiji cha Saunyi kilichoko Kilindi mkoani Tanga na maeneo mengine yakiwamo ya Kitwai Wilaya ya Simanjiro, Manyara. Juzi, wakati wa kuwaaga wananchi 596, Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro mkaoni Arusha, Kanali Wilson Sakulo alisisitiza kuwa zoezi la kujiandikisha na kuhama wananchi wa Ngorongoro ni la hiari na kwamba serikali itahakikisha kila mwananchi anayeitika wito huo kwa wakati, atapata haki zake zote anazostahili kwa mujibu wa sheria.

"Tunajua kwamba hivi karibuni kumekuwa na wimbi kubwa la upotoshwaji unaozunguka kwenye baadhi ya vyombo vya habari kuhusu zoezi hili, naomba mzipuuze habari hizo kwa kuwa nia ya serikali ni njema na inalenga kuboresha maisha yenu na mnapewa hiari ya kuchagua wenyewe mnakotaka kuhamia bila kushinikizwa," alisema Kanali Sakulo.

Kaimu Kamishna wa Uhifadhi wa NCAA, Victoria Shayo, alisema mamlaka hiyo inaendelea na utoaji wa elimu, uhamasishaji na uandikishaji wa wananchi. Kwa sasa mwitikio unaendelea kuongezeka na wananchi wengi zaidi wamefikiwa. Gladness Ngaluma, mmoja kati ya wananchi waliogwa, akizungumzia uamuzi huo, alisema yeye na familia yake wamechagua kuhamia Msomera kwa kuwa waliona huko watakuwa na uhuru zaidi wa kujiendeleza kwa kufanya shughuli za kiuchumi tofauti ni kuwa ndani ya hifadhi.

"Mimi na familia tumefanya uamuzi wa kuhama kwenda Msomera kwani huku hifadhini tunakosa uhuru wa kufanya maendeleo kama kujenga nyumba za kisasa, kilimo, kumiliki vyombo vya moto, uwepo wa wanyama wakali unaoathiri watoto kwenda shule hali iliyopelekea tuishi kwenye maisha duni," alisema Ngaluma.

# Wamarekani waipatia sekondari kompyuta

**Daniel Sabuni,** BABATI

TAASISI ya Wilderness Technology Alliance (WTA) ya nchini Marekani imetoa msaada wa kompyuta mpakato 20 zenye thamani ya shilingi milioni tano kwa Shule ya Sekondari ya Kwaraa iliyopo Wilaya ya Babati Mjini mkoani Manyara kwa ajili ya kufundishia masomo.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi kompyuta hizo juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa WTA, Lou August, alisema msaada huo ni mwanzo wa mradi wa taasisi yake kutoa kompyuta zaidi katika shule nyingi nchini. August, alisema kompyuta hizo za kujifunzia zinawafikia wanafunzi wengi ili wafikie malengo yao ya kusoma kutokana na urahisi wa kutumia teknolojia hiyo ya kisasa.

Alisema pamoja na kompyuta hizo, walimu 15 wa shule hiyo wanaofundisha masoma ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wamepewa mafunzo ya siku tano ya kutumia kompyuta kufundishia wanafunzi.

Vilevile, taasisi hiyo imetoa vifaa vingine vya TEHAMA ili kusaidia kuanzishwa kwa chumba maalum cha kisasa cha kufundishia masomo ya teknolojia hiyo.

Mratibu wa WTA nchini, Mwalimu Heke Gewe, alisema kompyuta hizo zina uwezo wa kutumika kama maktaba ya masomo badala ya vitabu kutokana na kuwekewa programu maalum za kisasa.

"Badala ya mabegi mazito yenye vitabu vingi vya kiada sasa wanafunzi wataingia maabara (darasa la kompyuta) wakiwa mikono mitupu na kupata elimu na kumpunguzia usumbufu mkubwa," alisema.

Alisema yeye na taasisi hiyo wamekuwa na uhusiano wa muda mrefu hadi kufikia kupanga mipango ya kubadilishana teknolojia kwa muda wa miaka mitano na sasa urafiki huo umezaa matunda ya kupata msaada wa kompyuta.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Babati, Halfa Matipula aliutaka uongozi wa shule hiyo kuhakikisha kompyuta hizo zinatunzwa na kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa ya kusaidia wanafunzi wengi zaidi.

"Walimu mliopata mafunzo haya ya TEHAMA mzingatie na muwe tayari kutumika katika sehemu nyingine za Wilaya ya Babati wakati wa mahitaji ukifika," alisema.

Ofisa Elimu Taaluma wa Wilaya hiyo, Tabu Mbaruku, alisema shule hiyo ina mchepuo wa TEHAMA, lakini wanafunzi walikuwa hawafanyi vizuri somo hilo kutokana na uchakavu, lakini sasa ana imani wataanza kufanya vizuri.

"Tunaomba ndugu zetu wa Wilderness, msiishie hapa Shule ya Sekondari Kwaraa, tuna shule za sekondari 21 katika Wilaya Babati, ambazo zina vyumba vya TEHAMA, lakini kompyuta hatuna, tuleteeni maana kompyuta ndiyo kila kitu kwenye elimu kwa sasa," alisema Mbaruku.

Mkuu wa shule hiyo, Degratius Michael, alisema msaada wa teknolojia hiyo umefika kwa wakati mwafaka kwa kuwa kompyuta hizo zitasaidia wanafunzi kusoma masomo mbalimbali badala ya kutumia vitabu.

Mmoja wa wanafunzi wa shule hiyo wa kidato cha kwanza, Gladness Mbise, alisema kompyuta hizo zitawasaidia kuelewa masomo kirahisi darasani badala ya kutumia vitabu.

"Endapo mwanafunzi hajamwelewa mwalimu wakati akifundisha baada ya kipindi, anaweza kwenda chumba cha maktaba akafungua kompyuta na kujisomea somo husika na akalielewa kwa urahisi zaidi," alisema.

Mwanafunzi mwingine, Christina Mmari wa kidato cha pili, alisema kompyuta hizo zitawasaidia kujisomea wakati umeme ukikatika kwa kuwa zina betri zinazomudu kutumika saa nne bila kuzimika.

# TIC: Watanzania wamechangia uwekezaji nchini

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

KITUO cha Uwekezaji nchini (TIC) kimesema kampeni ya nchi nzima ya kuhamasisha uwekezaji imeamsha ari ya Watanzania wengi kuchangamkia fursa za uwekezaji kwenye sekta mbalimbali.

Ofisa Uwekezaji wa Kituo hicho, Valentine Kagombora, aliyaeleza hayo juzi wakati akizungumza na wananchi waliotembelea banda la kituo hicho kwenye Maonyesho ya Biashara na Utalii yanayofanyika mkoani hapa.

Maonyesho hayo yaliyoanza Mei 28 yanatarajiwa kufungwa Juni 6 mwaka huu, kauli mbiu yake ni 'kufungua fursa za kiuchumi kupitia ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi' yamezishirikisha pia taasisi za umma.

Kagombora, alisema Tanzania ina fursa nyingi za uwekezaji, huku akihamasisha Watanzania kuunganisha nguvu ya mitaji na kusajili miradi ya ubia kwenye kituo hicho kama ambavyo wamekuwa wakifanya baadhi ya kampuni za kigeni.

Mwanzoni mwa mwaka huu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alizindua kampeni ya TIC kuzunguka mikoa mbalimbali nchini kuhamasisha uwekezaji wa ndani ambayo inatarajiwa kukamilika Septemba mwaka huu.

Kampeni hiyo inalenga kuhamasisha Watanzania kutumia fursa za uwekezaji zilizopo nchini na waache fikra kuwa uwekezaji ni kwa ajili ya wageni pekee.

Kagombora, pamoja na mambo mengine, aliwaeleza wananchi hao kuwa Tanzania imebarikiwa kuwa na fursa nyingi ambazo wanapaswa kuchangamkia na iwapo wataunganisha mitaji yao wanaweza kufanya mambo makubwa.

"TIC inaendelea na kampeni kwenye mikoa mbalimbali nchini ambako maofisa wa kituo wamekuwa wakikutana na wananchi kuwaeleza fursa zilizopo na namna ambavyo serikali inatoa kipaumbele kwa wawekezaji Watanzania," alisema.

Aliwaeleza wananchi hao kuwa serikali imepunguza kiwango cha mtaji kwa mwekezaji Mtanzania kutoka dola za Marekani 100,000 hadi dola 50,000 ili kuwawezesha wengi kuwekeza.

"Na tukisema dola 50,000 si kwamba ni fedha hapana, hii inajumlisha mtaji wake wote kuanzia mashine mitambo kama ni eneo la uwekezaji vyenye thamani kama hiyo na siyo fedha taslimu," alisema

Alisema TIC imekuwa ikifanyia kazi vikwazo vyote vya biashara kimoja baada ya kingine na lengo ni kuendelea kuwavutia wawekezaji wa nje na wa ndani ya nchi kuchangamkia fursa za uwekezaji.

Aliwataka Watanzania kusajili miradi yao kwenye kituo hicho kama unafuu wa kodi kwenye uingizaji wa mitambo na rasilimali za mtaji.

Amri Mohamed, ambaye alihudhuria maonyesho hayo, alisema ni vyema serikali ikaweka utaratibu wa kukutana na wafanyabiashara wa ndani mara kwa mara kuwapa elimu kuhusu uwekezaji kwani baadhi wanaamini ni kwa ajili ya wageni.

"Nimefurahi kuambiwa hata mimi naweza kuwa mwekezaji, sasa ni vyema elimu kama hii ikaendelea kutolewa nchi nzima ili Watanzania wengi wafahamu fursa za uwekezaji zilizopo ni kwa ajili yao pia siyo wageni pekee," alisema.







Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda (katikati), akifurahia jambo na Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri wa Bodi ya Maziwa, Prof. Zacharia Masanyiwa (kulia), na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Afia Sigge (kushoto), alipotembelea banda la benki hiyo katika maonesho ya 27 ya Wiki ya Maziwa yaliyomalizika jijini Mwanza mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Viongozi wa NCU kuwapaishia kiuchumi wakulima

**Na Vitus Audax,** MWANZA

VIONGOZI wa Bodi ya Chama Kikuu cha Ushirika Nyanza (NCU) 1984 wameahidi kuwainua wakulima wa pamba kiuchumi ili kuboresha maisha yao .

Ahadi hiyo waliitoa baada ya kuchaguliwa kuwa viongozi wa bodi hiyo katika Uchaguzi Mkuu wa chama hicho uliofanyika juzi jijini hapa.

Wajumbe hao waliochaguliwa katika uchaguzi huo kutoka kanda nane za kilimo cha pamba mkoani Mwanza ni Leonard William ni (Menyekiti), Mariamu Mashibe (Makamu Mwenyekiti), mwakilishi wa Nyanza nje ya bodi na wajumbe watatu.

Akizungumza baada ya kutangazwa mshindi, , William alisema kuwa watahakikisha wanakiingiza chama hicho katika soko la ushindani kwa na ununuzi wa mazao mchanganyiko na kuachana na utaratibu wa zao pekee la pamba.

"Mazao tutakayonunua tutalenga zaidi yale yaliyopo sokoni kama mpunga na mengineyo, tutaboresha na kufufua viwanda vya ushirika ili viweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuinua uchumi wa chama na wakulima kwa pamoja," alisema.

Kwa upande wake Mashibe, alisema watahakikisha wanakipatia ufumbuzi kilio kikubwa cha wakulima kukopwa bila kulipwa kwa muda mrefu na bei ndogo ya pamba.

Msimamizi wa uchaguzi huo, Leo Zephania ambaye pia ni Kaimu Mrajisi wa Ushirika Mkoa wa Mwanza, aliwataka viongozi hao wa bodi na wajumbe kusimamia mikakati ya kuiendeleza Nyanza.

"Mtapimwa kwa kazi mliyoifanya na pia ninyi wanachama shirikianeni vyema na wajumbe wa bodi ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao," alisisitiza Zephania.

# DC ashtukia 'upigaji' ujenzi Chuo cha Uuguzi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Mboni Mhita, ameshtukia ubadhirifu wa fedha za umma kwa kutokomilika kwa vyumba vinne vya madarasa vya Chuo cha Uuguzi katika Halmashauri ya Msalala kwa gharama ya Sh. milioni 180.

Mhita alibaini hayo juzi katika ziara ya kukagua miradi mbalimbali na kusema serikali imetoa Sh. bilioni 1.6 za ujenzi wa chuo hicho.

Alisema katika awamu ya kwanza, serikali ilitoa Sh. milioni 400 lakini mpaka sasa baadhi ya majengo, ikiwamo vyumba hivyo ujenzi wake hayajakamilika licha ya kuongezeka kidogo kwa ukubwa wake na kuchukua gharama ya Sh. milioni 45 kwa kila kimoja.

Alisema serikali kwa kushirikiana na wadau wamekuwa wakitekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo katika jamii, lakini kumekuwapo baadhi ya watendaji wake wasio waaminifu wanaotumia fedha za umma kujinufaisha na kuipa hasara.

Mhita alionya kuwa kuwa endapo watambaini mtumishi amekwamisha ujenzi huo atawajibika kwa mujibu wa sheria.

Mhandisi wa Halmashauri hiyo, Ramadhani Selemani, alisema mradi huo unapaswa kutumia kiasi cha Sh. bilioni 1.6, lakini fedha za awali zilitolewa ni Sh.milioni 400 ambazo zimetumika kujenga majengo mbalimbali.

Alisema, kati ya Sh.milioni 400 walizopokea Sh.milioni 220 zimetumika kujenga jengo la utawala na madarasa ya chuo yanayogharimu cha Sh.milioni 180 na sasa zimesalia Sh.milioni tisa .

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Judika Sumari, aliahidi kukamilisha mapungufu yaliyojitokeza katika ujenzi wa mradi huo.

Alisema mradi huo ulipaswa kuanza kazi katika msimu wa masomo wa mwaka 2023/2024, lakini imeshindikana kutokana na kutokamilika ujenzi wake kwa wakati.

# Askofu ataka uadilifu Jeshi la Polisi

**Na Neema Sawaka.** KAHAMA

ASKOFU Katoliki Jimbo la Kahama, Christopher Ndizeye amelitaka Jeshi la Polisi wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga kufanya kazi kwa uadilifu, kanuni na sheria katika utekelezaji wa majukumu yao ili kuwawezesha wananchi kuibua uhalifu na wahalifu kwenye maeneo yao.

Askofu Ndizeye alitoa wito huo juzi katika kikao kazi kilichoandaliwa na Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kahama, SSP Mtaju Mayombo kwa lengo la kuwakumbusha askari wajibu wa jeshi hilo na kujiweka wazi kwa raia.

Alisema wajibu wa jeshi hilo ni kuhakikisha jamii haipati manyanyaso , kupata haki zao na kuacha kufanya kazi kwa mazoea. SSP Mayombo alisema kuwa jeshi hilo lilianzisha polisi jamii ili kuliunganisha na wananchi na kufanya kazi zake kwa ufanisi . Askari polisi mstaafu, Thomas Muyonga ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kahama, aliwawataka askari hao kumtegemea Mungu katika utekelezaji wa majukumu yao ili kukabiliana na

# Mradi uvunaji maji ya mvua washika kasi Kishapu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

VIJIJI vya Miyuguyu na Mguda wilayani Kishapu Mkoa wa Shinyanga vinatarajia kuanza kunufaika na mradi wa uvunaji maji ya mvua na kuyahifadhi kwenye matangi ili kuondokana na adha ya kufuata maji umbali mrefu kipindi cha kiangazi.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kiuchumi na Jamii (ESRF), Profesa Fortunata Makene, wakati wa uzinduzi wa mradi huo ambao watautekeleza ndani ya miaka mitatu 2024 hadi 2027 baada ya kukamilika katika vijiji vitatu vya wilaya hiyo.

Prof. Makene alisema anatekeleza mradi huo katika vijiji hivyo viwili unakuja baada ya kufanya utafiti na kubaini wanawake wamekuwa wakipata shida kipindi cha kiangazi kwa kutafuta maji umbali mrefu wa kati ya kilomita 10 hadi 20 na kuacha kufanya shughuli za kiuchumi.

"Lengo la mradi ni kupunguza na kugawanya kazi zisizo na malipo kwa wanawake katika kuwawezesha kujikwamua kiuchumi ili wasipoteze tena muda sababu ya kufuata maji umbali mrefu," alisema.

Mkurugenzi wa Shirika la REDESO, Abeid Kasaizi, alisema wananchi watawezeshwa kuvuna maji hayo kwa kutumia paa za kwenye nyumba zao na kuyahifadhi kwenye matangi chini ya ardhi baada ya kuwajengea.

Kasaizi, alisema watajenga matangi 20 na kuziwezesha kaya 240 kupata maji safi na salama kipindi cha kiangazi.

Alivitaja vijiji hivyo vitatu ambavyo walianza kutekeleza mradi huo Kishapu mwaka 2021 ni Inolelo, Ngofila na Kiloleli.

Mkurugenzi Msaidizi wa Sera na Utafiti Wizara ya Maji, Alex Tarimo, alisema mradi huo ni miongoni mwa mikakati ya wizara kuhakikisha wananchi wanavuna maji ya mvua na kutumia wakati wa kiangazi.


Tarimo alitoa wito kwa wakazi wa Kishapu wenye nyumba za tembe kubadilika na kuanza kujenga nyumba za kisasa na kuezeka bati ili waweze kunufaika na mradi huo kwa kuvuna maji na kukabiliana na ukame.

Nipashe
Spotika



JURGEN Klopp amewaambia mashabiki wa Liverpool uamuzi wa kujiunga na timu hiyo kwake ilikuwa ni chaguo la pili katika maisha yake na sasa yuko tayari kuwaaga rasmi wapenzi wa klabu hiyo katika sherehe maalumu.

UKURASA 14




HAALAND

# HAALAND ACHEMKA KUFUNGA FAINALI 6

**MANCHESTER,** England

TANGU kuwasili kwake Manchester City mwaka juzi, Erling Haaland amekuwa ishara ya umahiri wa kufunga mabao na nguvu inayoongoza katika harakati za kutafuta utukufu.

Katika mwaka wake wa kwanza, raia huyo wa Norway alivunja rekodi ya ufungaji bora ya msimu mmoja wa Ligi Kuu England huku City ikinyakua mataji matatu.

Aliongoza safu ya ushambuliaji ya City kwa mara nyingine tena msimu huu walipopata taji la nne mfululizo la Ligi Kuu England.

Lakini licha ya mafanikio haya ya ajabu, kuna suala moja dhahiri katika taaluma ya Haaland hadi sasa; mara nyingi ameshindwa kufanya vyema katika fainali za mataji.

90min inatazama uchezaji wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 katika mechi sita za fainali za Manchester City.

Haaland alitoa mchango mkubwa katika kuelekea fainali ya Kombe la FA mwaka huu dhidi ya Manchester United, hasa akifunga mabao matano katika ushindi wa City wa 6-2 dhidi ya Luton Town katika raundi ya tano.

Kasi yake ya kufunga mabao ilisitishwa katika mchezo wa robo fainali dhidi ya Newcastle United ambapo alishindwa kufunga bao katika dakika 87 za mchezo wakati City iliposhinda 2-0, na alijeruhiwa kutokana na ushindi mdogo dhidi ya Chelsea hatua ya nusu fainali.

Kwa kuzingatia hali hizi, labda inaeleweka kwa nini Haaland alishindwa kupata bao dhidi ya United huku timu ya Pep Guardiola ikipoteza kwa kufungwa mabao 2-1.

**City 1-1 Sevilla (5-4 penalti) - UEFA Super Cup (Agosti 16, 2023)**

City walipata taji lao la kwanza la UEFA Super Cup kwa kuwashinda Sevilla 5-4 kwa penalti baada ya sare ya 1-1 kwenye Uwanja wa Georgios Karaiskakis mjini Piraeus.

Youssef En-Nesyri alianza kuifungia Sevilla kwa mpira wa kichwa kabla ya nyota wa sasa wa Chelsea Cole Palmer kufunga kwa kichwa ili kurejesha usawa.

Wakati Haaland hakupata wavu kwa muda wa kawaida - fowadi huyo hakufunga hadi kwenye penalti City ikiibuka washindi.

**Arsenal 1-1 Man City (4-3 penalti) - Ngao ya Jamii (Agosti 8, 2023)**

Haaland alicheza dakika 64 tu za pambano la City dhidi ya Arsenal kwenye Ngao ya Jamii msimu uliopita wa joto, na washikabunduki wakishinda 4-3 kwa penalti kufuatia sare ya 1-1 katika muda wa kawaida.

Nyota huyo alikuwa na mchezo wa chini chini, huku namba tofauti, Kai Havertz, akipata nafasi zaidi upande wa pili wa uwanja.

Cha kufurahisha ni City walifunga muda mfupi baada ya Haaland kutolewa nje Palmer alipopiga kona ya mbali.

**City 1-0 Inter - Ligi ya Mabingwa Ulaya (Juni 10, 2023)**

Ushindi wa kudumu wa City wa kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatimaye ulimalizika kwa ushindi wa 1-0 dhidi ya wababe wa Serie A Inter mjini Istanbul mwaka jana.

Kufuatia ushindi wao wa Ligi Kuu na Kombe la FA, City walipata bao dakika ya 68 likifungwa na Rodri.

Haaland alimaliza kampeni ya Ligi ya Mabingwa akiwa na mabao 12 kwa jina lake lakini hakufunga katika mechi zake tatu za mwisho.

**City 2-1 United - Kombe la FA ( Juni 3, 2023)**

Katika fainali ya kwanza kabisa ya Manchester City, bao la kufutia machozi la Ilkay Gundogan, liliiwezesha timu hiyo kushinda kombe dhidi ya Erik ten Hag.

Ingawa Haaland hakusajili bao au kusaidia katika shindano hili, alionyesha mchezo wa busara, akishikilia mpira kwa ustadi na kuusambaza kwa wachezaji wenzake bila ubinafsi.

**Liverpool 3-1 Man City - Ngao ya Jamii (Julai 30, 2022)**

Darwin Nunez aliibuka kidedea wakati Liverpool ilipoilaza City katika pambano la kusisimua la Ngao ya Jamii misimu miwili iliyopita.

Wakicheza kwenye Uwanja wa King Power badala ya Wembley, Wekundu hao walishinda mabao 3-1, shukrani kwa Trent Alexander-Arnold, Mohamed Salah na Nunez.

Aliyesajiliwa kutoka Borussia Dortmund mapema msimu wa joto kwa zaidi ya pauni milioni 50, Haaland alikuwa na mchezo wa kwanza kusahau kwani alikosa nafasi kadhaa. Onyesho la Mnorway huyo pia lilizidiwa na mchezaji mwenzake, Julian Alvarez, aliyeingia kama mchezaji wa akiba na kupachika lango la pekee la City.

Haaland alikuwa na miguso 16 pekee katika dakika zake 97 uwanjani, akimalizia pasi saba kati ya tisa alizojaribu kwenye mchezo.

## ISIKUPITE

KLABU mbalimbali zinazoshiriki Ligi Kuu ya Saudia maarufu Saudi Pro, ikiwamo Al Nassr, Al Ahli na Al Qasidiya, zinawania kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Brazil na Manchester United, Casemiro, mwenye umri wa miaka 32. (**Goal**)



NIPASHE JUMATATU JUNI 3, 2024





# WAAFRIKA WALIOWIKA EPL 2023/24

**LONDON,** England

PAZIA la Ligi Kuu England limefungwa kwa msimu wa 2023/2024, huku Manchester City ikiweka historia kwa kunyakua taji la nne mfululizo.

Miezi 12 iliyopita, Riyad Mahrez, alikuwa sehemu ya kusherehekea kombe la The Blues lakini baada ya winga huyo wa Algeria kuhamia Saudi Arabia, mabingwa hao hawana tena Mwafrika yeyote katika kikosi chao cha kwanza.

Hapa BBC Sport Africa imechagua wachezaji wachache kutoka barani kote ambao wamevutia macho kwa bora.

Baadhi wanaweza kuvutia soko la uhamisho, wakati wengine watakuwa na wasimamizi wapya wa kufanya kazi chini yao msimu mpya utakapoanza baadaye Agosti.

**Yoane Wissa (Brentford)**

Katika msimu wa kusikitisha kwa The Bees, mabao 12 ya Wissa yalikuwa muhimu sana katika kuepusha kushushwa daraja.

Kufikia kiwango chake bora zaidi England, aliongoza safu ya Brentford kwa ustadi kwa muda mrefu bila, Ivan Toney, aliyesimamishwa na kumjeruhi Bryan Mbeumo.

Fowadi huyo alifanikiwa yote licha ya kukosa mwezi mmoja wa msimu katika michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), ambapo aliisaidia Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), kutinga hatua ya nusu fainali kabla ya kushindwa na mabingwa na wenyeji, Ivory Coast.

Si mchezaji wa sehemu ndogo tena, itapendeza kuona ni kiasi gani mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 anaweza kuendeleza msimu ujao - hasa Toney akitarajiwa kuondoka.

**Nicolas Jackson (Chelsea)**

Mshambuliaji huyo wa Senegal alikuwa na msimu wa kwanza akiwa na Chelsea, ambao bado wana kazi kubwa licha ya kutumia Dola za Marekani bilioni 1.23 katika uhamisho tangu kununuliwa na Todd Boehly.

Jackson alifunga mara mbili pekee katika mechi zake saba za kwanza za ligi - huku akiendelea kufungiwa - kabla ya kufunga mabao matatu katika ushindi wa fujo dhidi ya wachezaji tisa wa Tottenham.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 alijitahidi kufanya vyema kati ya Novemba na Machi, mwaka huu lakini kiwango chake mwishoni mwa msimu, alifunga mabao manne huku Chelsea ikishinda mechi zao tano za mwisho, na kuashiria mustakabali mzuri kwa Mwafrika huyo wa Magharibi.

Hata hivyo, iwapo Kocha Mauricio Pochettino, atasalia dimbani au The Blues kuamua kusajili washambuliaji zaidi kunahatihati ya kuathiri muda wake wa kucheza Stamford Bridge.

**Mohammed Kudus (West Ham)**

Mghana huyo ameharibu sifa yake ya kuwa tishio baada ya uhamisho wa fedha nyingi kutoka Ajax.

Baada ya kipindi cha utulivu, Kudus alifikisha kilele cha ubora wa juu mnamo Desemba, mwaka jana na mtindo wake wa kipekee wa kusherehekea kufunga bao umemfanya awe kwenye ukumbi wa matangazo ya uwanja na kuwa jambo la kawaida kwa mashabiki.

Black Stars ilivumilia kuondolewa tena mapema AFCON lakini Kudus alimaliza akiwa na mabao 14 na pasi za magoli sita katika mashindano yote kwa The Hammers huku klabu hiyo ikikosa kucheza soka la Ulaya msimu ujao.

Julen Lopetegui anatazamiwa kuchukua nafasi ya David Moyes katika klabu hiyo ya London Mashariki na bila shaka Mhispania huyo atakuwa na nia ya kusalia na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 iwapo klabu kubwa zitamwita mara tu dirisha la uhamisho litakapofunguliwa.

**Antoine Semenyo (Bournemouth)**

Matokeo ya Bournemouth chini ya bosi mpya, Andoni Iraola, yalishangaza wengi na umbo la fowadi wa Ghana, Semenyo lilieleza mabadiliko hayo kikamilifu.

Haraka na bila kuchoka, aliwapa mabeki wakati mgumu na kuwa nyota kwa kuanza katika kila mechi.

Nyongeza ya mabao manane imekuwa wazi Bournemouth ilifanya biashara yenye tija ilipotumia pauni milioni 10, kumleta kutoka Bristol City Januari, mwaka 2023.

Uimara wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 pia



ADINGRA

Ubelgiji msimu uliopita, Simon Adingra, alifunga bao lake la kwanza kwa Brighton na kumalizia na mabao sita ya ligi.

Lakini utukufu wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 ulikuja na Ivory Coast kwenye AFCON, ambapo alifunga bao la kusawazisha dakika za lala salama kwenye robo fainali dhidi ya Mali na kisha kuweka mabao yote mawili kwenye fainali huku The Elephants wakinyakua taji lao la tatu la Afrika.


Mwanzoni mwa Aprili, Everton walikuwa wameshikilia rekodi ya klabu katika mechi 13 za Ligi Kuu ya England bila kushindwa na kuchupa kushuka daraja.

Wakati huo huo, hii ilikuwa kampeni ya Rayan Ait-Nouri, alikomaa na kujigeuza kuwa chaguo la kwanza kwa Wolves na Algeria.

Tishio kubwa mbeleni, beki huyo wa kushoto mwenye umri wa miaka 22 amehusishwa na uhamisho wa kwenda timu tatu zilizopigania taji msimu huu.

## Nukuu

"Tunafuraha sana kushinda kombe hili. Historia, utamaduni wa klabu, wachezaji, ukweli klabu hii ni familia. Tuna mazingira bora na tunafanya kazi kwa ushirikiano bila ya matatizo. Wachezaji wanajituma na wanajitoa kwa ajili ya klabu. Haikuwa jambo gumu kuongoza kikosi hiki msimu huu." **Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amesema baada ya kutwaa ubingwa wa Ulaya.**



'England inaweza kutwaa ubingwa wa michuano ya Euro 2024. Nafikiri kikosi tulichonacho sasa kinayafanya mataifa mengine yaanze kutuhofia kwa kaisi fulani," **nahodha wa zamani wa timu hiyo, Wayne Rooney, amesema hayo kuelekea mashindano hayo yatakayofanyika hivi karibuni nchini Ujerumani.**



"Kama nilitaka kwenda huko, nisingekuwa hapa, ninapenda kucheza soka. Ni wazi kwamba fedha pia ni muhimu lakini nina ndoto ya kumalizia soka langu katika Ligi Kuu England," **Son, mshambuliaji wa Tottenham alisema hayo kumaliza uvumi hana mpango wa kuelekea Saudi Arabia.**






Kiungo mshambuliaji wa Simba, Clatous Chama, msimu huu tena yupo katika rada za kutakiwa na Yanga. Tayari waajiri wake wamemwekea dau mezani ambalo bado hajaridhishwa na huenda ikawa njia ya kujiunga na Yanga. **PICHA: MTANDAO**

# TETESI 11 ZA USAJILI ZINAZOTIKISA BONGO

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara imemalizika, tayari baadhi ya timu zimeshaanza mchakato wa kusaka wachezaji wapya kwa ajili ya msimu ujao.

Na hii haipo hapa nchini tu, hata Ulaya na kabla ya hapo, klabu zipo kwenye mikakati ya kusajili wachezaji ili kuongezea nguvu vikosi vyao.

Hapa nchini tetesi mbalimbali zimeanza kusikika kwa baadhi ya wachezaji kutoka klabu moja kwenda nyingine. Pia viongozi wa timu baadhi yao, akiwamo Rais wa Yanga, Hersi Said, walisafiri nje ya nchi, ambapo pamoja na mambo mengine ni kuhakikisha wanapata nyota wazuri kwa ajili ya msimu mpya.

Katika makala hii tutaangalia tetesi za usajili zinazovuma kwa sasa na majina ya wachezaji wanaotajwa kuhamia kwenye klabu mpya.

### 1. Mayele kutua Simba SC

Tetesi hizi zilianza tangu katikati ya msimu wa ligi kipindi cha dirisha dogo, lakini kuelekea mwishoni mwa ligi, straika huyo wa zamani wa Yanga, ambaye kwa sasa anaichezea Pyramids ya Misri, anatajwa kutaka kuhamia Simba.

Zipo habari zinasema nyumba aliyokuwa akiishi straika, Jean Baleke ambaye ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo kama ilivyo Fiston Mayele, imeandaliwa kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye uwezo wa kufumania nyavu.

### 2. Kinzumbi atajwa Yanga

Winga machachari wa TP Mazembe, Phillipe Kinzumbi, anatajwa atatua kwa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga kuanza kazi kuelekea msimu mpya.

Tetesi zinasema safari ya Hersi huko DRC na viongozi wa TP Mazembe kuja nchini, pamoja na mambo mengine ilikuwa ni harakati za mabadilishano ya wachezaji kwa timu zote mbili.

Inasemekana Yanga imekubali kumwachia, Kennedy Musonda, ambaye alitakiwa sana na TP Mazembe wakati alipokuwa Power Dynamos, lakini ikamkosa na kutimkia Yanga, lakini kwa sasa itampata kwa makubaliano rasmi.

Yanga inadaiwa kutoa mchezaji huyo pamoja na fedha kidogo kwa ajili ya kumpata Kinzumbi.

### 3. Lyanga kutimkia Simba

Inaelezwa Ayoub Lyanga amegomea mkataba mpya na Azam FC, chanzo kikisema anataka kujiunga na Simba ambako pamoja na dau la usajili, lakini wamemwekea mshahara wa Sh. milioni 10 kwa mwezi.

Mkataba wa mchezaji huyo na Azam utatamatika mwishoni mwa msimu.

### 4. Chama mguu Simba, mguu Yanga

Nyota wa Simba, Mzambia, Clatous Chama, inatajwa huenda akajiunga na Yanga msimu ujao kama Simba hawatamwongeza dau analohitaji.

Tetesi zinasema, mchezaji huyo anahitaji kulipwa Sh. milioni 700 ili asaini mkataba mpya, lakini klabu imegoma na imemwekea ofa ndogo ambayo inaamini inamfaa kutokana na umri pamoja na uwezo wake wa sasa.

Chanzo kinasema klabu imemwambia kama anaona ndogo basi anaweza kwenda popote anapoona anaweza kuipata pesa hiyo, huku taarifa zinasema hiyo ni habari nzuri kwa Yanga ambayo inamwania kwa misimu kadhaa.

Mpaka sasa kuna hamsini kwa hamsini, anaweza kubaki Simba, au kwenda Yanga.

### 5. Mkude anabakia Yanga

Kuna mazungumzo ambayo yamefikia pazuri kati ya menejimenti ya kiungo mkabaji, Jonas Mkude na uongozi wa Yanga kwa ajili ya kuongeza mkataba mpya wa kusalia kwenye klabu hiyo.

Mkude ambaye alisaini mkataba wa mwaka mmoja na Yanga akitokea Simba, ameonekana kuwavutia mabosi wa klabu hiyo mpya, hasa katika mechi za mwisho za Ligi Kuu na michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

### 6. Kibwana atakiwa Simba

Beki wa kulia wa Yanga ambaye ana uwezo wa kucheza upande wa kushoto, Kibwana Shomari, anaonekana kuwindwa na Simba kwa ajili ya kwenda kumsaidia, Shomari Kapombe.

Kibwana ambaye anamaliza mkataba wake mwishoni mwa simu huu, inasemekana waajiri wake wa sasa hawajafikia dau analohitaji, hivyo inaweza kurahisisha mchakato wake wa kutua kwa Wekundu wa Msimbazi.

### 8. Kagoma abadili gia angani

Kiungo mkabaji aliye katika kiwango cha juu msimu huu, Yusuph Kagoma wa Singida Fountain Gate, awali alitajwa kuhitajika Yanga kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano.

Hata hivyo, Simba iliingia kati dili na mwenyewe akabadilika, akitaka kwenda kucheza Msimbani kwa kile kilichoelezwa ni wepesi wa kupata namba.

### 9. Lawi wa kwanza Simba

Tetesi zinasema beki wa kati ya Coastal Union, Lameck Lawi, ndiyo wa kwanza kusajiliwa na Simba msimu huu.

Habari zinasema alisaini wiki mbili zilizopita kuichezea klabu hiyo kwa miaka miwili.

### 10. Matampi awakuna Simba

Uwezo wa golikipa Mkongomani, Ley Matampi, umeonekana 'kuwakuna' viongozi wa Simba, ambao sasa wameonyesha nia ya kutaka kumsajili.

Kipa huyo aliyesajiliwa na Coastal Union na kusimama langoni mechi 16 bila kuruhusu bao akimpiku kipa wa Yanga, Djigui Diarra, anaonekana anaweza kuisaidia timu hiyo ambayo imeonekana kuruhusu mabao mengi msimu huu.

### 11.Mwamnyeto lulu Simba

Viongozi wa Simba wanatajwa kumhitaji beki wa kati ya Yanga, Bakari Mwamnyeto ili kuongeza nguvu ya ulinzi pale kati. Beki huyo ambaye Simba ilimkosa miaka kadhaa iliyopita alipokuwa Coastal Union na kutua Yanga, bado yupo vichwani kwa mabosi, wakiamini atawasaidia, huku mkataba wake wa timu yake ya sasa ukitamatika.

Habari zinasema Simba imeweka dau kubwa mezani, kuliko la Yanga ambalo wamempa mchezaji wao.

## JE, WAJUA?



JURGEN Klopp amewaambia mashabiki wa Liverpool uamuzi wa kujiunga na timu hiyo kwake ilikuwa ni chaguo la pili katika maisha yake na sasa yuko tayari kuwaaga rasmi wapenzi wa klabu hiyo katika sherehe maalumu.



# Makaburi yang'olewa misalaba kwa ajili ya vyuma chakavu

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

WAKAZI wa Kata ya Chang'ombe jijini Dodoma wamelalamika kukithiri kwa ung'oaji wa misalaba kwenye makaburi unaodaiwa kufanywa na vijana wauza vyuma chakavu.

Wakizungumza na waandishi wa habari kwa nyakati tofauti, mmoja wa wakazi hao, Hamis Ramadhani alidai kuwa kwenye makaburi yaliyopo kwenye kata hiyo, misalaba yote iliyotengenezwa kwa chuma, imeng'olewa na vijana hao na kuuzwa kama vyuma chakavu.

Ramadhani alidai kuwa vijana hao pia wamekuwa wakibomoa zege na kuchukua nondo kisha kwenda kuziuza kwenye chuma chakavu.

Alidai kuwa kutokana na uharibifu huo, ndugu wanaofiwa na kuzika kwenye makaburi hayo, wamekuwa wakiwawekea alama ya mawe na misalaba ya mbao ambayo imekuwa ikiliwa na mchwa.

"Inatusikitisha sana kutokana na vitendo hivyo ambavyo ni sawa na udhalilishaji wa ndugu zetu wanaokufa kwa kuibiiwa alama zao ambazo ni muhimu kwa kumbukumbu za kujulisha walipozikwa ndugu zao," alilalamika Ramadhani wakati akizungumza kwa niaba ya wenzake.

Alisema kwenye kata hiyo ya Chang'ombe, biashara ya vyuma chakavu imekithiri na imekuwa kama ajira kwa vijana ambao wanarandaranda mitaani kuiba sufuria, sahani na bakuri zilizotengenezwa na bati.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mazengo iliyopo katika kata hiyo, Abdallah Mtosa alithibitisha kukuthiri kwa vitendo hivyo vinavyofanywa na vijana hao kwa lengo la kujipatia vyumba kisha kwenda kuuza kama vyuma chakavu.

Mtosa, alisema vijana hao wamekuwa waking'oa misalaba ikiwamo ile inayotengenezwa kwa zege na kuchukua nondo.

Alisema wakazi wa kata hiyo, wamewasilisha malalamiko ofisini kwake na kuomba serikali kuwadhibiti vijana hao kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi.

"Nikiwa Mwenyekiti wa Mtaa wa Mazengo Jiji la Dodoma, nipo karibu na makaburi hayo, wananchi wamenileteа taarifa ya kuwapo kwa uharibifu huo wa kung'olewa kwa misalaba hiyo na vijana wanaodhaniwa kuwa ni wauza vyuma chakavu," alisema.

Alisema vijana hao, pia wamekuwa tabia ya vijana ya kukaa vijiweni wakicheza kamari na michezo ya kubeti badala ya kutumia muda wao kuzalisha uchumi kinyume na sheria.




Mbunge wa Nyasa, Mhandisi Stella Manyanya, akimpa chakula mtoto wa tembo kwenye maonesho ya Wizara ya Maliasili na Utalii yanayoendelea viwanja vya Bunge jijini Dodoma mwisho wa wiki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Biteko: Mpango mafuta, gesi ukamilike haraka

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, ameagiza mpango wa matumizi wa mafuta na gesi ukamilike haraka ili uweze kutumika kuwahudumia wananchi.

Agizo hilo alilitoa juzi jijini hapa wakati wa uzinduzi wa mpango wa matumizi bora ya nishati na matumizi ya magari yanayotumia umeme.

Dk. Biteko aliwaagiza viongozi wanaosimamia mpango huo wa mafuta na gesi ukamilike haraka ili uweze kutumiwa na wananchi.

Alisema mpango wa mafuta na gesi upo katika mchakato wa kukamilika, hivyo viongozi wanatakiwa kuharakisha mchakato huo ili uweze kukamilika na kuanza kutumika.

Alisema ni lazima mipango yote isomane ili isilete sintofahamu yoyote katika utendaji wake.

Alitaka jamii kuendelea kushirikiana na serikali katika juhudi za kutunza mazingira na miradi iliyopo na inayotarajiwa kuanzishwa. Aliongeza kuwa baada ya kuzindua kituo hicho anatarajia vituo vingine vitazinduliwa katika maeneo ya mikoani.

Naibu Waziri Mkuu huyo, alisema amefurahishwa na jinsi Umoja wa Ulaya (EU) na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) zinavyoendelea kutoa misaada kwa Tanzania katika miradi ya maendeleo na kuyahakikisha nishati hiyo inawafikia wananchi.

Mwakilishi wa EU, Lamine Dialo, alisema umoja huo utaendea kusaidia miradi ya matumizi bora ya nishati nchini.

Dialo, alisema lengo la mashirika hayo kutoa nishati hizo ni kulinda mazingira na kuleta nafuu ya matumizi ya nishati katika matumizi mbalimbali.

Mwakilishi wa UNDP, Shigeki Komatsubara, alisema wataendelea kuhakikisha mazingira yanaendelea kutunzwa nchini kwa kusaidia miradi nchini.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, aliyashukuru mashirika hayo na kuwakaribisha wadau wengine kutumia jua la Dodoma kuzalisha nishati ya umeme.

# RC ahimiza uwekezaji kumbi za mikutano

**Na Paul Mabeja,**
DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amesema baada ya kuanza kutumika kwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Msalato mwakani mkoa huo utakuwa na uwezo wa kupokea mikutano ya kimataifa.

Senyamule aliyasema hayo juzi jijini hapa kwenye Maadhimisho ya Miaka 20 ya Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo (SACCOS) cha Kanisa la Kiinjili la Kirutheri (KKKT) Usharika wa Arudha Road Dodoma.

Alisema kutokana na uwekezaji unafanya na serikali ya awamu ya sita mkoani hapa, ikiwemo ujenzi wa uwanja huo wa ndege, fursa nyingi zitajitokeza, watu binafasi na taasisii nchini kuchangamkia.

"Nyie kama SACCOS tayari mnao mtaji, ni wajibu wenu kuchangamkia fursa hii kwani mkoa wetu mradi huu ukikamilika utakuwa na uwezo wa kumiliki mikutano ya kimataifa hivyo tutapa wageni wengi.

"Tutumie fursa hizi kwa kuwekeza katika sekta mbalimbali ikiwemo hoteli kubwa za kimataifa, kumbi za mikutano kwani hivi sasa hatuwezi kuwa na mikutano ya kimataifa wakati hakuna kiwanja cha ndege cha kisasa, hivi sasa lazima wageni kutoka nje lazima washuke kwanza Dar es Saalam ndipo waje hapa, lakini ikikamilika Msaloto watatua moja kwa moja hapa Dodoma," alisema Senyamule.

Mwenyekiti wa Bodi ya SACCOS hiyo, Ibrahimu Sumbe, alisema wazo la kuanzisha chama hicho lilitoka kwa wafanyakazi wa usharika huo chini ya Mchungaji Fuataeli Munisi.

Alisema wafanyakazi hao waliamua kuwa na umoja wa kuchangiana kila mwisho wa mwezi kwa mzunguko.

"Baadaye wakaona ni vyema waanzishe SACCOS, kwa ajili ya wafanyakazi wa Usharika. Yote haya yalikuwa yanafanyika katika harakati za kupiga vita umaskini," alisema. Alisema wakati taratibu za kuanzisha SACCOS zikiendelea Ofisi ya Usharika iliona ni vyema kuwashirikisha waumini.

Hata hivyo, alisema mtaji wa chama hicho umeendelea kukua kutoka Sh. milioni 1.7 mwaka 2004 kilipoanzishwa rasmi hadi kufikia Sh. bilioni 1.06 Aprili mwaka huu.



# Halmashauri yatwishwa zigo kulipa walimu wa kujitolea

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe mkoani hapa wameitaka halmashauri hiyo kutenga fedha kwa ajili ya kuwalipa walimu wa kujitolea na kuwapunguzia gharama wazazi.

Wito huo waliutoa wiki iliyopita baada ya kuibuka hoja hiyo katika kikao cha baraza la madiwani uliofanyika katika ukumbi wa halmashauri hiyo.

Baadhi ya madiwani walisema umefika wakati kwa halmashauri hiyo kuingilia kati kwa kuanza kuwalipa walimu wa kujitolea kwa manufaa ya watoto badala ya kuwaachia wazazi na walezi na kusababisha wengi wao kushindwa kumudu gharama kutokana na ukosefu wa kipato.

Isaya Myamba, Diwani wa Igongolo, alisema walimu wa kujitolea wanafanya kazi nyingi, lakini malipo yao hawapati kwa wakati.

"Ili kuweza kuwalipa hao walimu kwa mfano shule za msingi ukitenga bajeti kuwalipa 200,000 wa shule 50 kwenye halmashauri yetu unakuta ni shilingi milioni 240 kwa mwaka sasa mnaonaje ili suala mkalibeba," alisema Myamba.

Innocent Gwivaha, Diwani wa Matembwe, alisema ili walim hao waweze kufundisha vizuri ni lazima halmashauri iwape motisha.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Melkizedeck Kabelege, alimwagiza mkurugenzi kufanyia kazi suala hilo ili kukabiliana na uhaba wa walimu katika shule nyingi na kuinua kiwango cha elimu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Christopher Sanga, alisema amepokea maelekezo hayo na kuahidi kwenda kukaa na wataalamu wake ili kujadili kukabiliana na hali hiyo na kuhakikisha kiwango cha elimu kinaendelea kupanda.

"Sisi kama CMT haturidhishwi na hali ya elimu ya sasa Njombe ile ya zamani tuliwapata viongozi wengi, jitihada zinahitajika ili kunusuru elimu," alisema Sanga.

Hata hivyo, alionya tabia ya walimu wanaopangwa kufundisha katika shule za halmashauri hiyo kuomba kuhama kwa kile kinachotajwa kuwa ni vijijini.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Mary Makondo (kushoto), akimsikiliza Mkazi wa Njombe, Tulafiwona Sempagani, alipofika kwenye vibanda vya kutoa huduma ya msaada wa kisheria kupitia Kampeni ya Huduma ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia inayoendelea mkoani hapa hivi karibuni. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wazazi wakumbushwa kuhudumia watoto

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAZAZI na walezi katika Kijiji cha Luponde kilichopo Halmashauri ya Mji Njombe mkoani hapa wametakiwa kuzingatia elimu ya lishe na kutenga muda wa kuwahudumia watoto wao baadala ya kujikita zaidi kujitafutia kipato.

Wito huo ulitolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Kuruthum Sadick kwenye Siku ya Afya na Lishe ya Kijiji (SALIKI) iliyofanyika katika kijiji hicho.

"Tujitahidi kuwa na muda kamili wa kuwahudumia watoto, tukifundishwa tukayachukua halafu tusiyazingatie itakuwa ni kazi bure, kazi tufanye lakini tupate muda wa kuhudumia watoto," alisema.

Aliongeza kuwa: "Niwaombe wamama wa Njombe, ninaelewa ni watafutaji kwelikweli, asubuhi kabla hujaenda shamba hakikisha unamwandalia mtoto wako lishe iliyo bora," alisema Sadick.

Alibainisha kuwa ili kuondokana na vitendo vya ukatili kwa watoto ni lazima mama kuwa na muda wa kuzungumza na watoto wake na kuwafanyia uchunguzi katika miili yao mara kwa mara.

"Licha ya kuwalisha watoto tunaona vitendo vibaya vinafanyika kwa watoto, mnashuhudia wenyewe watoto wanabakwa, watoto wananajisiwa, hii ni kwa sababu wamama tumewaacha watoto wetu hatuna muda nao," alisema.

Mkurugenzi huyo aliwaomba wazazi waliopatiwa elimu hiyo kufikisha kwa waume zao na kuhakikisha wanaanzisha bustani za mboga mboga nyumbani ili kuwa na uhakika wa upatikanaji lishe bora kwenye mlo wa familia.

Kwa upande mwingine, alimtaka mtendaji na ofisa kilimo wa Kata ya Luponde kushirikiana na uongozi wa kijiji kutoa elimu ya kulima bustani jiko ili jamii ihamasike kupanda mbogamboga nyumbani.

Wakizungumza baada ya elimu hiyo, Mary Msigwa, alisema wataizingatia elimu hiyo ingawa wanakabiliwa na tatizo la wanaume kuwatelekezea watoto.

"Hapa ukiangalia wanawake wengi wanahudumia familia wenyewe na muda wa kukaa na watoto kweli hakuna, lakini tutajitahidi kwahudumia watoto wetu," alisema Msigwa.

Hali ya udumavu katika halmashauri hiyo imepungua kwa asilimia 3 kutoka 45 Desemba 2022 hadi kufikia 42 mwaka 2024.

# TBS yatoa somo kwa watumiaji vipimo

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WATUMIAJI vipimo katika mazingira na shughuli zao wametakiwa kujifunza matumizi sahihi ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na ukuaji wa teknolojia.

Kauli hiyo ilitolewa wiki iliyopita na Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Profesa Othman Chande kwenye Maadhimisho ya Siku ya Viwango Duniani yalifanyika jijini hapa yenye kauli mbiu "Vipimo kwa Uendelevu."

Profesa Chande alisisitiza kuwa ni muhimu wa kutumia vipimo katika uzalishaji mali na biashara ili kukabiliana na mabadiliko hayo yanayoendelea kutokea sehemu mbalimbali duniani na kuleta athari za kiuchumi.

"Nawashauri wazalishaji, mamlaka za usimamizi wa ubora, mahospitali, wafanyabiashara na wananchi wote kutumia vipimo sahihi ili tuweze kukuza na kutunza mazingira yetu na uchumi wetu," alisema.

Alisema matumaini yake baada ya maadhimisho hayo wataendelea kuchukua hatua stahiki katika matumizi bora ya vipimo kwa uendelevu.

Kwa mujibu wa Prof. Chande, maadhimisho hayo yanawakumbusha kuhusu umuhimu wa vipimo sahihi kushughulikia changamoto za kijamii, kimazingira na kiuchumi.

Alisema TBS wamepewa dhamana na Serikali ya kutunza vipimo kitaifa, hivyo wana jukumu la kuunda na kudumisha viwango vya upimaji vya kitaifa ambavyo ni msingi wa vipimo sahihi na vya kuaminika katika nyanja mbalimbali.

"Maadhimisho haya yanatukumbusha kutoa ushauri wa kuaminika kwa serikali, taasisi na mashirika ya udhibiti na sekta mbalimbali kuhusu masuala yanayohusiana na vipimo kwa uendelevu," alisema.

Mkurugenzi wa Upimaji na Huduma za Metrolojia wa TBS, Ridhiwan Matange, alisema maadhimisho hayo wanawakumbusha umuhimu wa vipimo sahihi katika maisha ya kila siku ya mwanadamu, mathaani kwenye afya kuanzia manunuzi ya chakula, uandaaji wa chakula na ulaji.

Matange, alisema TBS maabara yake ya metrolojia imepewa dhamana ya kutunza viwango kitaifa na kutoa usababishaji wa vipimo hivyo, kuwakilisha nchi katika masuala ya vipimo na kutoa huduma ya ugenzi.

Alisema vipimo ni msingi wa maendeleo vinawapatia takwimu na taarifa muhimu zinazohitajika ili kufanya maamuzi sahihi, kuendeleza vumbuzi na kuhakikisha maendeleo endelevu ndani ya jamii.





# ACT yampongeza Samia, yawatangazia kiama mafisadi 2025

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha ACT-Wazalendo kimempongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuisaidia Zanzibar kupata udhamini wa miradi ya ujenzi visiwani hapa yenye thamani ya mamilioni na kutangaza kiama dhidi ya wanaokwamisha utekelezaji na mafisadi kitaposhika dola mwakani.

Pongezi hizo zilitolewa na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Ismail Jussa katika mkutano wa hadhara uliofanyika Uwanja wa Geji Bububu Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja mwishoni mwa wiki iliyopita.

Jussa, alisema mradi wa mkakati ulikuwa ujenge barabara ya Mkoani/Chakechake, Uwanja wa Ndege Pemba, barabara ya Tunguu/Makunduchi na Kisauni/Fumba kwa kutumia mkopo uliodhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Uingereza.

"Zanzibar imetaka mkopo kwa ajili ya kujenga uwanja wa ndege wa kisasa Pemba, kwa ajili ya kuitengeneza barabara ya Chake hadi Mkoani, Tunguu hadi Makunduchi, barabara mbadala kutoka Fumba hadi Kisauni na jumla ya mradi wa kimkakati ilikuwa sio rahisi kwa Serikali ya Muungano kutoa udhamini wa mkopo ule mkubwa lakini Serikali ya Mama Samia imetoa udhamini," alisema.

Alisema kujengwa kwa uwanja huo na barabara ya Chakechake kungeifungua kiuchumi kisiwa hicho cha Pemba, lakini mradi huo umekwama tangu Novemba mwaka jana na kampuni ya ujenzi ya kizalendo ndio waliokuwa wameshinda zabuni ya utekelezaji wa mradi huo.

"Katokea kiongozi mmoja anadai rushwa kupitia fedha za mradi huo, walipokataa kavuruga mradi mzima," alisema.

Akizungumzia ubinafsishaji wa Shirika la Bandari Zanzibar tangu kukabidhiwa wawekezaji kutoka Ufaransa, alisema hakuna uboreshaji wowote wa huduma zaidi ya gharama za uzalishaji kuendelea kupanda na kuwaumiza wananchi.

Alisema kwa mujibu wa bajeti ya matumizi na mapato ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ya mwaka wa fedha 2024/2025, shirika hilo linakusudia kukusanya mapato ya shilingi bilioni 37 wakati matumizi yake ni shilingi bilioni 7 kwa mwaka.

Alidai kuwa mradi wa ujenzi wa jengo la pili la abiria kwenye Uwanja wa Abeid Amani Karume unafanyika kinyume na sheria kwa sababu fedha hazijaidhinishwa na Baraza la Wawakilishi na hakuna zabuni iliyotangazwa jambo ambalo ni kinyume na sheria.

Mwenyekiti wa Chama hicho, Othman Masoud, alisema viongozi na watumishi wanaotuhumiwa kwa ubadhirifu na mikataba ya kifisadi wafunguliwa mashtaka baada ya ACT kushika madaraka mwaka 2025 na kuburuzwa mahakamani.

"Rasilimali za nchi hii zinatakiwa zitumike inavyotakiwa, kama umeiba kukufunga tutakuja kukufunga sisi maana tunajua nyie wenyewe hamuwezi kufungana," alisema na kusisitiza kuwa: "Sisi tunawaambia aliyehujumu mali ya serikali, aliyeingia mikataba ya kifisadi, aliyekwapua kila pahali mkono wake tutaukata, tutahakikisha anafikishwa kwenye vyombo vya sheria na atakayethibitika atafungwa, mwenyewe nimedumu katika vyombo vya sheria kwa miaka 18." Othman aliwahi kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar. ACT-Wazalendo kimeanza mikutano ya hadhara jimbo kwa jimbo ambayo wameipa jina bandika bandua.

Mikutano hiyo itafanyika katika majimbo 50 ya Zanzibar, ambayo tangu kuanza kwake viongozi wake wamekuwawakitumia muda mwingi kukosoa misingi ya demokrasia na utawala bora na vitendo vya ufisadi vinavyojitokeza katika miradi ya ujenzi Zanzibar.



Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mhandisi Cyprian Luhemeja (kulia), akiongozana na Katibu Tawala Mkoa wa Geita, Mohamed Gombati, kufanya usafi wa mazingira katika eneo la Hospitali ya Rufani ya Kanda- Chato mkoani Geita ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Usafi wa Mazingira kitaifa juzi. **PICHA: ISMAIL NGAYONGA**

# Wananchi wengi Zanzibar hawajui sheria

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba, Sheria, Utawala Bora na Utumishi wa Umma, Mzee Ali Haji, amesema wananchi wengi visiwani hapa kutofahamu sheria isiwe kigezo cha kushindwa kuhukumiwa kwa makosa ya uvunjifu wa sheria.

Haji alitoa kauli hiyo jana wakati akifungua mafunzo ya uelewa wa muongozo wa uanzishwaji wa vituo vya msaada wa kisheria katika vyuo vikuu na vituo vinavyotoa mafunzo ya msaada wa kisheria visiwani hapa.

Alisema wananchi wengi wa Zanzibar wanakabiliwa na changamoto mbalimbali hasa uwelewa mdogo wa sheria zinazotungwa visiwani hapa ikizingatiwa kuna sheria nyingi zinafanyiwa mabadiliko, lakini jamii haizifahamu.

Alisema jamii inakabiliwa na changamoto kubwa ya sheria ya ardhi hasa katika umiliki kiasi ambacho wahusika wengi kukosa haki zao kwa kutozijua na kukithiri kwa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Haji, alisema idara ya msaada wa kisheria, imekuwa ikifanya kazi kubwa ya kuwaelimisha wananchi wa mijini na vijijini juu ya uwepo wa msaada wa kisheria, lakini peke yao haitoshi kufanya kazi hiyo.

Alisema katika kufikia malengo ya uwepo wa idara ya msaada wa kisheria, ipo haja ya kuwafundisha baadhi ya wasaidizi ili wananchi kufahamu haki na wajibu wao katika majukumu yao ya kila siku.

Mkurugenzi wa Idara ya Msaada wa kisheria wa Wizara hiyo, Hanifa Ramadhan Said, alisema wanatoa elimu kwa makundi mbalimbali ili wawe mabalozi wazuri kwa jamii iliyowazunguka.

Hanifa, alisema mafunzo hayo yataendelea kutolewa na idara hiyo kupitia washirika wake wa maendeleo ikiwamo shirika linaloshughulikia masuala ya Wanawake UN WOMEN chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU).

Akitoa maada katika mafunzo hayo juu ya sheria ya mahakama ya kadhi namba 8 ya mwaka 2023, kadhi kutoka Wilaya ya Madharibi B Unguja, Hemed Saleh Ali, alisema itaondoa msongamano wa kesi zikiwamo za madai ya talaka mahakamani na kutoa ufanisi wa kazi.

Ali, alisema kwa sasa jamii inakabiliwa na changamoto katika masuala ya ndoa hasa mgawanyo wa mali zilizochumwa na wanandoa baada ya kuachana.

# 'Umaskini isiwe chanzo watoto wa kike kukosa elimu'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISA Mradi wa Jinsia kutoka Taasisi ya kutengeneza mazingira safi kwa mtoto wa kike (KFHI), Grace Maseo Laizer, amesema umasikini katika jamii usiwe sababu kwa wazazi kuwakosesha watoto wa kike kupata elimu.

Akizungumza katika mafunzo juu ya usawa wa kijinsia kwa wazazi wa Kijiji cha Paje Wilaya ya Kusini Unguja, Laizer alisema kuwa wazazi wanatakiwa kufahamu kumsomesha mtoto wa kike ni moja ya faida kubwa kwa taifa na hivi sasa dunia inamtazama mtoto huyo kama ni mtaalamu kama wataalamu wengine.

Alisema licha ya watoto wa kike kukabiliwa na changamoto nyingi katika kipindi cha kutafuta elimu, bado imeonekana kuwa baadhi ya wazazi wanachangia jambo ambalo sio sahihi.

Laizer, alisema wazazi wengi wana mtazamo wa mfumo dume katika jamii zao kwa kupenda kumsomesha mtoto wa kiume ambao kwa sasa umepitwa na wakati.

Alisema watoto wa kike wakikoseshwa katika jamii wana fursa nyingi ikiwa ni pamoja na kuandaliwa kuwa mama wa familia na kwamba mtazamo huo ni wa kibaguzi na ukandamizaji wa haki.

Alisema wakati umefika kwa wazazi hasa katika maeneo ya ukanda wa pwani kuwapa nafasi ya kusoma watoto wa kike ili kukamilisha ndoto zao za baadaye.

Meneja wa Shirika la KFHI, Taewan Park, alisema elimu ya jinsia ni msingi wa kujenga jamii jumuishi kwa mtoto wa kike na kiume bila ya kujali tofauti zao za kimaumbile.

Alisema wameanza kuungana na serikali kutengeneza mazingira rafiki ya kujisomea kwa wanafunzi hasa wa kike ili kukamilisha ndoto zao za kuwa viongozi wazuri bora kwa baadaye.

Akifunga mafunzo hayo ya mwezi mmoja kwa wazazi hao, Ofisa Elimu Wilaya ya Kusini Unguja, Mussa Nahoda Makame, alisema licha ya serikali kuwa mstari wa mbele katika kuwahimiza mtoto wa kike kusoma bado kuna changamoto ndani ya jamii hasa wazazi kuwa na mitazamo iliyopitwa na wakati.

Alisema wazazi wengi wa Zanzibar wamekuwa wakiogopa kuwagombeza watoto wao wanapofanya makosa, jambo ambao sio.

Alisema watoto wa kiume wanakabiliwa na changamoto ya ajira za utotoni hasa katika sekta ya uvuvi kwa kisingizio cha hali ya umasikini.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

IRENE BAHATI NDOWO anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye usajili namba MC 364 BBW. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/22925/2023

## KUPOTEA KWA CHETI



JOHN IBRAHIM MWAKALINDILE anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S2501/0036/2018 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia KIJIBA SECONDARY SCHOOL mwaka 2018. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIG/100709/2024

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE
Kituo cha JUMUISHI
Mkoa DAR ES SALAAM
Usimamizi wa mirathi Na 778 /2024

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SHABAN YUSUFU MWAKIMWAGILE WA KINONDONI
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ABUBAKARI SHABANI MWAKIMWAGILE

TANGAZO
(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 21 mwezi 06 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia:
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe 30 Mwezi 05 Mwaka 2024

HAKIMU

---

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF TEMEKE DISTRICT
(ONE STOP JUDICIAL CENTRE)
AT TEMEKE
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 26243 OF 2023
IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE THERESIA EMMANUEL MASSAWE
IN THE MATTER OF APPLICATION FOR THE LETTER OF ADMINISTRATION BY ARDESIA KIMARO MASSAWE.

NOTICE TO CREDITORS

(Made under Rule 111 of the probate Rules)

NOTICE is hereby given that all persons claiming debts or liabilities affecting the estate of the above named THERESIA EMMANUEL MASSAWE, deceased who died at MUHIMBILI NATIONAL HOSPITAL, ILALA DISTRICT DAR ES SALAAM REGION on the 27TH APRIL 2023 and probate of whose letters of administration of whose estate were granted to me by the court on the 15th Day of MAY 2024, are hereby required to send in their claims to me via phone 0787366919 within sixty (60) days from the date of the publication of this notice at the expiration of which time I shall proceed to hand over the assets to the process entitled thereto having regard to the claims of which I shall then have had notice.

ARDESIA KIMARO MASSAWE
ADMINISTRATIX
PHONE: 0787356919
DISTRICT: MBEZI, MSAKUZI MWISHO
REGION: DAR ES SALAAM

---

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
Probate and Administration Cause No 19 of 2024
In the matter of the estate of the late MASIMA DAUDI PAULO of Chanyika within Dodoma City
And
In the matter of application for letter s of administration by HILDA DAUDI PAULO
GENERAL CITATION
(Rule 75 of probate Rules GN NO. 369 of 1963)

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on before the 11 day of 06......... 2024.

Dated at Dodoma this 13 day of 05.........2024.

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE DODOMA

.........................................
RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI NA BAJAJI

FIKI RI UDUGU MBEGU anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki zenye usajili namba; MC 521 BYZ, MC 921 CPQ, MC455BQG , T 698 BKU na MC 882CQC na kadi za bajaji zenye usajili namba MC 827 AEA, MC 367 BZM, MC 738 CLS , MC 710 CBZ na MC 909 CHG. Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/94248/2024

## KUPOTEA ZA KADI ZA PIKIPIKI NA GARI

CHARL ES PHILIPO GWICHA anatangaza kupoteza kadi za pikipiki zenye usajili namba MC 343 CVR (TVS), MC 484 CUZ (BOXER), MC 505 CMH (TVS), MC 384 DGK (BOXER), MC 974 DUS (BOXER), MC 478 DUR (BOXER), MC 812 DGT (TVS), MC 109 DGK ( BOXER) , MC 136 CZK (BOXER) na kadi ya gari aina ya TOYOTA PASSO yenye usajili namba T 531 DTM. Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
PHQ/DAR/KIN/103873/2024
PHQ/DAR/KIN/103880/2024

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

AMEDEUSI AROBOGASTI MASAWE anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC356DEV, aina ya HAOJUE. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

TAARIFA YA POLISI: PHQ/DOD/DOD/17244/2024

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

AMEDEUSI AROBOGASTI MASAWE anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC751DQQ. aina ya HAOJUE. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya Polisi: PHQ/DOD/DOD/17244/2024

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA
MAHALI DODOMA
MAOMBI MADOGO NA. 303 YA MWAKA 2024
BAINA YA
EMMY SHAYO ........................................ MDAI
DHIDI YA
EMANUEL SUDAY ..................................... MDAIWA

KWA:EMANUEL SUDAY
POPOTE ULIPO

YAH: KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 25.06.2024 saa 3:00 asubuhi. Kwa ajili ya hukumu.

ANGALIZO: Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu. Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 30 ya mwezi Mei, 2024.

MWENYEKITI
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

HILARY ABEL MSIGWA anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba MC 494 CJD, CHASSIS NAMBA: LC6PCJK0058159 na ENGINE NAMBA: 156FMI5AD2F57082. Kwa yeyote atakaeione atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: PHQ/RUV/SON/2952/2024


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0677020701**

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industrial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Mshirika wa Khamenei ajisajili kuwania urais Iran

**TEHRAN,** Iran

KAMANDA wa zamani wa kikosi cha walinzi wa mapinduzi ya Iran aliyewekewa vikwazo na Marekani Vahid Haghanian, ni miongoni mwa wagombea waliojisajili kugombea nafasi ya urais iliyoachwa wazi baada ya kifo cha Ebrahim Rais.

Haghanian, ambaye ni mshirika wa karibu wa kiongozi wa juu wa Iran Ayatollah Ali Khamenei, alisema kwamba, anastahili kuwa katika nafasi hiyo hasa baada ya uzoefu wake wa miaka 45 katika ofisi ya rais na ya kiongozi mkuu.

Spika wa zamani wa bunge Ali Larijani, Gavana wa zamani wa benki kuu nchini humo Abdolnaser Hemmati ni miongoni mwa watu 12 waliojisajili kugombea nafasi hiyo.

Hemmati alisema kikubwa atakachokifanya akipata nafasi hiyo ni kutumia diplomasia kuondoa vikwazo vya kiuchumi dhidi ya Iran na kuwa na mahusiano mema na nchi za nje.

"Juhudi zangu zote zitaelekezwa katika kufanya kazi na majirani zetu, kutanua ushirikiano wa kiuchumi na nchi zote zinazoweza kufanikisha masilahi yetu ya kitaifa. Nitatumia pia diplomasia kuondoa vikwazo na kuwa na mahusiano na ulimwengu wa nje," alisema Hemmati.

Baada ya usajili wagombea watachujwa na Baraza la viongozi wa kidini. **DW**

# Indonesia iko tayari kutuma majeshi kulinda amani Gaza

**SINGAPORE CITY**

RAIS mteule wa Indonesia, Prabowo Subianto, amewaambia wajumbe wanaohudhuria mkutano wa usalama duniani kwamba nchi yake iko tayari kutuma wanajeshi wa kulinda amani kusaidia utekelezaji makubaliano ya kusitisha mapigano ya ukanda wa Gaza pindi yakapoafikiwa.

Mkutano huo ni wa kila mwaka unajulikana kama Jukwaa la Majadiliano ya Usalama la Shangri-La ambao unawaleta pamoja maofisa wa usalama duniani unafanyika kwenye mji mkuu wa Singapore, Singapore City.

Mwaka huu majadiliano yametawaliwa zaidi na mzozo wa Gaza, vita vinavyoendelea kati ya Ukraine na Russia pamoja na suala la usalama kwenye kanda ya Bahari ya Hindi na Pasifiki.

Rais Prabowo alikuwa akizungumzia pendekezo la kusitisha mapigano la awamu tatu lililotolewa na Rais wa Marekani Joe Biden.

Pendekezo hilo kiongozi wa Indonesia kundi la Hamas linalotawala Ukanda wa Gaza limesema linatia moyo na linalitafakari limetoa matumaini ya uwezekano wa kumalizwa vita vilivyodumu kwa zaidi ya miezi saba.

Chini ya mpango huo Biden alisema Israel imependekeza hatua tatu muhimu za kumaliza vita.

Hatua ya kwanza itakuwa ni kipindi cha wiki sita cha usitishaji mapigano ambacho kitashuhudia vikosi vya Israel vikiondoka kwenye miji yote iliyo na watu wengi kwenye Ukanda wa Gaza.

Hatua ya pili na ya tatu itajumuisha kubadilishana mateka wote na wafungwa na baadaye vikosi vya Israel vitaondoka kikamilifu na mpango wa kuijenga upya Gaza utaanza.

Rais Prabowo alisema pendekezo hilo ni hatua iliyopigwa katika mwelekeo unaostahili.

"Ingawa inabidi tuangalie na kuchunguza kwa makini kilichopo ndani ya pendekezo hili lililotangazwa na Rais Joe Biden, lakini tunaliona kama hatua muhimu iliyochukuliwa katika kusonga mbele," alisema kiongozi huyo ambaye bado anashikilia wadhifa wa waziri wa ulinzi wa Indonesia.

Prabowo alisema iwapo wataombwa na Umoja wa Mataifa (UN) kuchangia katika hatua za kusitisha mapigano basi wako tayari kutuma kikosi cha kulinda amani kusimamia utekelezaji makubaliano ya kusitisha mapigano pamoja na kutoa ulinzi na usalama kwa pande zote zinazohasimiana.

Prabowo aliyeshinda urais katika uchaguzi wa mapema mwaka huu anatarajiwa kuchukua wadhifa huo mwezi Oktoba mwaka huu kuongoza taifa hilo lenye idadi kubwa zaidi ya waislamu duniani.

Jukwaa la Shangri-La pia litakuwa uwanja mwingine wa kujadili hali ya usalama duniani inayotiwa kiwingu na vita kati ya Rassia na Ukraine.

Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, naye alihudhuria mkutano wa Jukwaa la Shangri-La akilenga kuvutia uungwaji mkono wa kimataifa kwa utawala wake mjini Kyiv katika vita vinavyoendelea.

Ilielezwa kuwa aliwasili kwenye ukumbi wa mikutano akiwa na maofisa kadhaa wa ulinzi kutoka kila pembe ya dunia wanaoshiriki mkutano huo, huku akitarajiwa kulihutubia jukwaa hilo.

Pia aliandika kwenye ukurasa wake wa mtandao wa X kwamba "nitafanya mikutano kadhaa, ikiwamo na Rais wa Singapore Tharman Shanmugaratnam na Waziri Mkuu Lawrence Wong, Rais wa Timor Jose Ramos-Horta, Waziri wa Ulinzi wa Marekani Lloyd Austina na wawekezaji wa Singapore".

Zelensky amekuwa akifanya ziara kwenye mataifa ya Ulaya siku za karibuni kuomba misaada ziada ya kijeshi kwa ajili ya askari wake katikati mwa hujuma nzito za Russia inayosonga mbele kwenye uwanja wa vita.

**DW**



Wapalestina wakikimbia na mali zao huku moshi ukifuka kwa nyuma katika kitongoji cha Tel al-Sultan Rafah, kusini mwa ukanda wa Gaza juzi. **PICHA: AFP**

# Uchaguzi Madagascar wagubikwa na sintofahamu

**ANTANANARIVO,** Madagascar

SIKU tatu baada ya uchaguzi wa wabunge nchini Madagascar ambao ulilenga kurejelea nafasi za wabunge 163 ndani ya Bunge la taifa, Shirika la Safidy, ambalo ni ujumbe wa waangalizi wa uchaguzi nchini humo, umesema uchaguzi huo uligubikwa na matukio ya kutisha.

Pamoja na waangalizi wake waliotumwa katika karibu vituo 4,000 vya kupigia kura kati ya 28,000 nchini humo, Safidy inaonyesha hali ya kwanza ya jumla, ikieleza kuwa watu wengi walishiriki katika uchaguzi wakiwamo wanasiasa lakini hali haikuwa sawa.

Msemaji wa shirika hilo, Carinah Rahaivojaonina, alisema wapigakura waliruhusiwa kupiga kura mara kadhaa, wengine wakipiga bila vitambulisho, wagombea walitoa pesa au chakula kwa wafuasi wao, ikiwa ni baadhi ya kasoro zilizobainishwa na Shirika la Safidy siku ya uchaguzi.

"Safidy itawasilisha maombi na kushughulikia hali kwa msingi wa kesi kwa kesi kulingana na ushahidi ambao tutapokea kutoka kwa waangalizi ambao bado wako katika maeneo mbalimbali nchini.

"Kwa hivyo bado hatuwezi kutoa maoni kuhusu kama hii itaathiri matokeo ya uchaguzi au la," alisema.

Katika ripoti yake ya awali, uchunguzi huo kwa mara nyingine unahoji kutoegemea upande wowote, kutopendelea na kujitegemea kwa Ceni, Tume ya Uchaguzi inayohusika na kuandaa kura.

Ilielezwa kuwa CENI ilikabiliwa na ukosoaji mkali haswa kutoka kwa upinzani wakati wa uchaguzi wa urais wa mwaka 2023.

Msemaji wa pili wa Shirika la Safidy, Stella Razanamahefa, alisema Madagascar pia inalaumiwa kwa kujihusishanavitendovilivyoashiria kutokuwa na usawa kati ya wagombea.

"Jambo lingine ambalo tumeweza kulieleza ni ushirikishwaji wa watumishi wa serikali na chama waliopo madarakani, hasa wakuu wa mikoa, wilaya au watumishi wa wizara.

"Huwa ni tatizo katika kila uchaguzi kwa sababu vyama vilivyopo madarakani vinahusika na wafanyakazi hawa katika kampeni zao za kawaida, jambo ambalo husababisha kukosekana kwa usawa wa fursa kati ya wagombea," alisema.

Hata hivyo ilieleza kuwa ujumbe wa uchunguzi haujakamilika, huku wananchi wengi wanaohusishwa na Safidy wakiangalia kwa umakini mkubwa uchambuzi na uchakataji wa taarifa za uchaguzi zinaofanyika hivi sasa katika sehemu tofauti za sensa ya vifaa vya kupigia kura kisiwani humo. **RFI**

# IHEFU YAJITOSA KUMWANIA STRAIKA TEGEMEO WA KMC

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Ihefu FC imeanza harakati za usajili, na tayari jicho lake limeelekea kwa kinara wa mabao ya KMC katika Ligi Kuu Tanzania Bara iliyomalizika, Waziri Junior, imefahamika.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo ambayo imehamia mkoani Singida, zinasema mchezaji huyo ni moja kati ya mapendekezo ya benchi la ufundi yenye lengo la kuimarisha safu yao ya ushambuliaji.

Chanzo kinasema Ihefu inalazimika kufanya usajili mkubwa kwa sababu malengo yake ya msimu ujao ni kupata nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa baada ya kushuhudia msimu uliomalizika ikishindwa kumaliza ndani ya 'Top Four'.

"Tumeazimia kusajili wachezaji wachache, lakini wenye ubora mkubwa, tumepatwa na huzuni kubwa timu kama Coastal Union kwenda kucheza mechi za kimataifa halafu timu yetu imeikosa, kwa hiyo tutafanya usajili mkubwa na wa maana, tutakuwa na wachezaji wachache lakini wenye viwango vya juu," kilisema chanzo hicho.

**Habari zinasema Waziri anatakiwa kwenda kumsaidia straika tegemeo kwa sasa katika timu hiyo, Elvis Rupia ambaye ni raia wa Kenya.**

Waziri Jr amemaliza msimu uliopita akiwa na mabao 12, akishika nafasi ya tatu, nyuma ya Feisal Salum 'Fei Toto' wa Azam FC aliyefunga magoli 19 huku kiatu cha dhahabu kikichukuliwa na Stephane Aziz Ki wa Yanga, alizifumania vyavu mara 21.

Kwa msimu uliomalizika, ndiye straika pekee aliyeongoza kwa kufunga mabao mengi.

Habari kutoka ndani ya Ihefu pia zinasema klabu hiyo ipo katika mazungumzo na kiungo mkabaji, raia wa Sierra Leone, Mohammed Kamara, kutoka klabu ya Hameenlinnan Jalkapalloseura ya Finland.

"Mkataba wake na timu yake unafikia ukingoni msimu huu, tumemwambia asisaini tena, tunamhitaji," kilisema chanzo hicho.

Kiliongeza katika kujiimarisha, watacheza mechi mbalimbali za kirafiki na timu za ndani na nje ya Tanzania.

"Tunajua msimu mpya mambo yataendelea kuwa magumu, kila siku ligi yetu inazidi kuimarika, hakuna mechi rahisi na lolote linaweza kutokea kama utabweteka," kiliongeza chanzo chetu.

Hata hivyo bado Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), halijafungua rasmi dirisha la usajili.



Baadhi ya watoto wakishiriki programu ya michezo kwa lengo la kuibua vipaji iliyofanyika kwenye viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam jana na kudhaminiwa na wadau mbalimbali ikiwamo Maji ya Kilimanjaro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# JKU yakaribia kutwaa ubingwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

JKU SC imeendelea kujiimarisha katika mbio za kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Wanajeshi wa Hard Rock FC katika mchezo wa raundi ya 27 ya ligi hiyo uliochezwa juzi.

Kwa matokeo hayo, JKU imefikisha pointi 62 wakati wapinzani wao wa karibu KMKM yenye pointi 54 wakikubali kufungwa mabao 2-1 na Mafunzo SC huku.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa JKU, Salum Ali Haji, alisema anaamini timu yake ina matumaini makubwa ya kushinda taji hilo.

Haji alisema anahitaji kupata pointi sita katika mechi tatu zilizobakia ili kukamilisha msimu huu.

Alisema matarajio yake makubwa ni kuona michezo mitatu iliyobaki anashinda yote ili hata kama wapinzani wao watashinda bado kikosi chake kitatimiza malengo.

"Tunaendelea kuwapa hamasa wachezaji wetu, hamasa ambayo kila mmoja katika timu yetu wamehamasika sehemu kubwa katika mbio hizi za ubingwa," alisema kocha huyo.

Nafasi ya tatu katika msimamo wa ligi hiyo inashikiliwa na Zimamoto yenye pointi 52, lakini imecheza mechi moja pungufu.

## Nyota Simba, Twiga Stars washiriki kliniki

**Na Mwandishi Wetu**

WADHAMINI wakuu wa Ligi Kuu Bara, Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), wameendesha programu ya michezo kwa watoto yenye lengo la kuibua vipaji sambamba na kuhamasisha wazazi kuweka akiba kwa ajili ya watoto wao. Hatua hiyo ni mwendelezo wa mkakati wa benki hiyo katika kukuza sekta ya michezo nchini kupitia vipaji sambamba kutoa huduma jumuishi za kifedha kwa makundi yote wakiwamo watoto.

Katika kufanikisha programu hiyo iliyofanyika kwenye viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam jana, benki hiyo ilihusisha wadau mbalimbali wakiwamo wachezaji wa Simba, Shomari Kapombe, Mzamiru Yassin, Ladaki Chasambi na Hussein Abel huku nyota kutoka Twiga Stars wakiwa ni Stumai Abdallah na Fatuma Issa 'Fetty Densa'.

Kupitia programu hiyo NBC ilikabidhi zawadi mbalimbali kwa washiriki zikiwamo jezi pamoja na mipira huku ikishuhudiwa watoto hao wakipata wasaa kushiriki mazoezi maalumu chini ya usimamizi wa wachezaji wakongwe waliohudhuria.

Meneja Masoko wa NBC, Alina Kimaryo, alisema kupitia programu hiyo inayotarajiwa kufanyika mara tatu kwa mwaka inalenga kuhusisha watoto wenye umri kati ya miaka sita na 13.

"Benki ya NBC tunaamini katika imani kwamba kesho nzuri inaandaliwa leo. Kupitia programu hii ya kliniki ya mchezo ya Chanua Akaunti tunaandaa kesho nzuri kwa watoto kupitia vipaji vyao hususani vya kimichezo kwa kuzingatia ukweli michezo ni ajira.

Pia tunaandaa kesho ya watoto kupitia kuhamasisha wazazi wajenge utamaduni wa kuweka akiba kwa ajili ya watoto wao na hiyo ndio sababu hapa unaona kuna vyote viwili yaani michezo na elimu ya fedha na akiba kwa wazazi," alisema Kimaryo.

Akizungumzia elimu ya fedha na malezi ya watoto, Msimamizi wa Huduma za Elimu wa NBC, Yoabu Ndanzi, alisema pamoja na kuwajengea uwezo na maarifa wazazi kuhusiana na umuhimu wa kuwawekea akiba watoto wao, pia programu hiyo inalenga kuwajengea uwezo wa kutambua umuhimu wa michezo na vipaji.

"Tunashukuru kuona wazazi wengi katika darasa hili tayari wana uelewa wa kutosha kuhusu kuweka akiba ndio maana tayari wameshafungua akaunti za Chanua kwa ajili ya watoto wao. Tunajitahidi zaidi kuwaelewesha kuhusu kutambua umuhimu wa michezo na vipaji vya watoto wao kwa kuzingatia ukweli michezo ni ajira.

Tulianza na wachezaji wa Azam FC, leo (jana) tumewaleta wa Simba na tukio lijalo tutawaleta wachezaji wa Yanga na watafuatiwa na wachezaji wa timu nyingine pia," Ndanzi alisema.

Kapombe alisema amefurahi kushiriki katika programu hiyo kwa sababu inasaidia kukuza na kuwaandaa vyema wachezaji.

"Zaidi kwa kuwa programu hii inahusisha wazazi tunaamini kabisa itasaidia kubadili mitazamo yao kuhusu suala zima la kuheshimu vipaji vya watoto wao," alisema Kapombe.

Tima Mohamed, mmoja wa wazazi walioshiriki alisema amevutiwa na programu hiyo kwa sababu inahusisha maeneo muhimu na yenye manufaa kwa watoto ikiwamo michezo, elimu ya fedha na kuweka akiba na afya.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CITY KUMFUNGA HAALAND
KLABU ya Manchester City imeweka kipaumbele cha kumfunga mshambuliaji wa Norway, Erling Haaland, mwenye umri wa 23, kwa mkataba mpya. (***Mirror***)

### FAYE WA BARCA SOKONI
ARSENAL imewasilisha maombi kwa Barcelona kuhusu upatikanaji wa mlinzi wa Timu ya Taifa ya Senegal, Mikayil Faye, mwenye umri wa miaka 19. (***Mail***)

### ARSENAL YAMTAKA SSEKO
ARSENAL wanataka kupata saini ya mshambuliaji wa RB Leipzig na Slovenia, Benjamin Sesko, mwenye umri wa miaka 21, kabla ya kifungu chake cha uhamisho cha euro milioni 65 kukamilika ifikapo Juni, mwishoni. (***Florian Plettenberg***)

### PSG YAIANGUKIA NAPOLI
KLABU ya Paris St-Germain inataka Napoli ipunguze thamani yao ya euro milioni 100 kwa Khvicha Kvaratskhelia, huku wakitaka kufikia makubaliano ya mshambuliaji huyo wa Georgia mwenye umri wa miaka 23. (***L'Equipe*** )

### FOFANA ATAKIWA ENGLAND
KLABU ya Monaco iko tayari kumuuza kiungo wa kati wa Ufaransa, Youssouf Fofana, anayelengwa na Arsenal na Manchester United kwa pauni milioni 20, huku kandarasi ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 ikikamilika mwaka ujao. (***Goal***)

### FELIX KUREJEA BARCELONA
KOCHA wa Barcelona, Hansi Flick, ameonyesha nia ya kumsajili tena, Joao Felix, mwenye umri wa miaka 24 kwa mkopo kutoka Atletico Madrid licha ya winga huyo wa Ureno kushindwa kuwa na kiwango bora kabisa huko Nou Camp chini ya Xavi. (***Marca***)

### WITSEL, ATLETICO SAFI
KIUNGO wa kati wa Ubelgiji, Axel Witsel, mwenye umri wa miaka 35, ambaye amekubali kustaafu kucheza michuano ya Euro, anataka kusaini mkataba mpya na Atletico Madrid baada ya kuwa na msimu mzuri akicheza kama mlinzi wa kati. (***Fabrizio Romano***)

### KELLY ANUKIA NEWCASTLE
NEWCASTLE United imebakia katika mazungumzo na Bournemouth kuhusu mpango wa kumnunua mlinzi wa England, Lloyd Kelly, mwenye umri wa miaka 25, baada ya kumkosa beki wa Fulham, Tosin Adarabioyo (26), ambaye anatazamiwa kufanyiwa vipimo vya afya na Chelsea. (***Sky Sports***)

### HESABU ZAKATAA UNITED
KLABU ya Manchester United ina uhaba wa pauni milioni 30 katika hesabu yao kwa mlinzi, Jarrad Branthwaite, mwenye umri wa miaka 21. (***Football Insider***)

### BERG KUONDOKA LIVERPOOL
MLINZI wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Sepp van den Berg, mwenye umri wa miaka 22 ameomba kuondoka Liverpool ifikapo msimu huu wa joto. (***De Telegraaf***)

### MOURINHO NA FORMOSINHO
JOSE Mourinho ataungana na msaidizi wake wa zamani, Ricardo Formosinho, ambaye alifanya naye kazi Manchester United na Tottenham Hotspur, baada ya kukubali kutua katika kikosi cha Fenerbahce. (***Telegraph*** )

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KIMMICH AKERWA NA UBAGUZI UJERUMANI

**Kiungo huyo asema soka linaunganisha mataifa, dini...**

**MUNICH,** Ujerumani

KIUNGO wa kati wa Ujerumani, Joshua Kimmich, ameelezea uchunguzi ambao uligundua moja kati ya raia watano wenzake wangependelea zaidi wachezaji weupe kwenye Timu ya Taifa kama „ubaguzi kabisa."

**Kura ya maoni ya washiriki 1,304 waliochaguliwa bila mpangilio iliidhinishwa kwa ajili ya filamu ya hali halisi ya Shirika la Utangazaji la ARD „Umoja, haki na tofauti," ambayo itaonyeshwa kesho kutwa.**

Asilimia 21 ya waliohojiwa walisema wangependelea wachezaji wengi wenye ngozi nyeupe kuichezea Ujerumani.

„Mtu yeyote ambaye amekulia na soka anajua huu ni upuuzi mtupu. Soka hasa ni mfano mzuri wa jinsi unavyoweza kuunganisha mataifa tofauti, rangi tofauti za ngozi na dini tofauti," alisema Kimmich, ambaye ni mzungu.

„Hivyo ndivyo timu yetu inavyohusu. Huu ni ubaguzi wa rangi kabisa na hauna nafasi katika chumba chetu cha kubadilishia nguo."

Kimmich alikuwa akizungumza huko Herzogenaurach, ambapo Ujerumani imeweka kambi ya mazoezi kwa ajili ya michuano ijayo ya Ulaya.

Kikosi hicho cha wachezaji 27 kinajumuisha wachezaji sita weusi.

„Unapofikiria tunakaribia kuandaa mashindano ya Ulaya nyumbani, ni upuuzi kuuliza swali kama hilo wakati lengo ni kuunganisha nchi nzima," alisema Kimmich.

„Inahusu kufanikisha mambo makubwa pamoja. Kama timu, tunajaribu kupata kila mtu nchini Ujerumani nyuma yetu."

Ujerumani inajiandaa kwa michuano ya Euro 2024 kwa mechi za kirafiki dhidi ya Ukraine itakayochezwa leo mjini Nuremberg na nyingine dhidi ya Ugiriki itakayofanyika siku nne baadaye huko Mönchengladbach.

Ujerumani itafungua dimba Juni 14, mwaka huu kwa kuwakaribisha Scotland mjini Munich, kisha itacheza dhidi ya Hungary mjini Stuttgart mnamo Juni 19 na Uswizi huko Frankfurt mnamo Juni 23, mwaka huu.

HABARI MICHEZO

# Chelsea yaachana na Osimhen

**LONDON,** England

CHELSEA kwa sasa haimwanii tena mshambuliaji wa Napoli, Victor Osimhen, huku kukiwa na wasiwasi juu ya gharama ya mkataba huo, kulingana na ripoti.

Osimhen ameonekana kwa muda mrefu kama mshambuliaji anayelengwa na Chelsea, huku The Blues wakimfuatilia nyota huyo mwenye umri wa miaka 25 kwa takribani miaka miwili sasa.

Uhamisho msimu huu wa joto ulionekana kukwama wakati aliposaini mkataba mpya wenye kipengele cha kuachiliwa chenye thamani ya zaidi ya pauni milioni 100.

Lakini kwa mujibu wa Fabrizio Romano, bei hiyo imechangia uamuzi wa Chelsea kupunguza nia yao kwa Osimhen.

The Blues bado wanatarajiwa kusajili mshambuliaji mpya msimu huu wa joto lakini watatafuta mbadala wa bei nafuu na si Osimhen.

Chelsea ni miongoni mwa timu zinazomwania, Benjamin Sesko wa RB Leipzig huku pia wanatazamia kuuza washambuliaji wachache ambao wamesajiliwa kwa sasa wakati Romelu Lukaku na Armando Broja wakipatikana kwa uhamisho msimu huu wa joto.

Lukaku anapatikana kwa pauni milioni 38 baada ya kumalizika kwa mkopo wake na Roma na hivi majuzi alisemekana analengwa na miamba ya Uturuki Fenerbahce.

Kuhusu Broja, Chelsea walikuwa wakidai pauni milioni 50 ili kuinasa saini ya mhitimu huyo wa akademi yao hapo Januari.





# KROOS AONDOKA MADRID NA TAJI LA SITA LA UEFA

**LONDON,** England

TONI Kroos aliita rekodi yake ya mataji sita ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ni "wazimu" baada ya kumaliza maisha yake ya klabu kwa kuisaidia Real Madrid kutwaa Kombe lao la 15 la Ulaya katika ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Borussia Dortmund kwenye Uwanja wa Wembley, juzi usiku.

Kroos mwenye umri wa miaka 34, alitangaza mapema mwaka huu atastaafu soka baada ya kuiwakilisha Ujerumani kwenye Euro 2024 na kufanya fainali ya Ligi ya Mabingwa kuwa mchezo wake wa mwisho akiwa amevalia jezi ya Real Madrid.

Na baada ya kutengeneza bao la ufunguzi la Dani Carvajal kabla ya kubadilishwa kwa shangwe, Kroos alijiunga na gwiji wa Real, Paco Gento na wachezaji wenzake wa sasa Carvajal, Luka Modric na Nacho wakiwa na rekodi ya mataji sita ya Ligi ya Mabingwa.

Kroos alisema hakuamini ukubwa wa mafanikio yake binafsi ya ajabu.

"Inashangaza," alisema Kroos akiiambia CBS.

"Mataji sita ya Ligi ya Mabingwa ni wazimu, kitu ambacho sikuwahi kufikiria ningekipata."

Kroos alishinda Ligi ya Mabingwa ya kwanza kati ya sita akiwa na Bayern Munich dhidi ya Dortmund huko Wembley mwaka 2013, lakini ameongeza la tano akiwa na Real Madrid.

Na alisema klabu hiyo ya Hispania ina hisia tofauti linapokuja suala la kucheza Ligi ya Mabingwa.

"Inaonekana katika michezo hii, hatuwezi kupoteza," Kroos alisema. "Hutapoteza fainali. Huo ni msingi mzuri kuwa nao nadhani.

"Inatokea kwa sababu ya ubora, bila shaka, lakini mawazo ni ya kichaa. Ni kuamini sana. Ndio jambo linalotenganisha klabu hii na wengine.

"Inaweza kuwa mbaya zaidi. Huo ulikuwa mpango [wa kumaliza na ushindi wa Ligi ya Mabingwa], ingawa ni vigumu kupanga hili."

# Konate: Msinihusishe na PSG

**LIVERPOOL,** England

BEKI wa kati wa Liverpool, Ibrahima Konate, amesisitiza kujitolea kwake katika klabu hiyo licha ya kuhusishwa na uhamisho mpya wa kwenda Paris Saint-Germain.

Konate, ambaye alizaliwa Paris, amekuwa akidokezwa kwa muda mrefu kurejea katika mji mkuu huo wa Ufaransa na alifanya kila awezalo kupunguza uvumi huo Novemba, mwaka jana.

Lakini, anapoingia miaka miwili ya mwisho ya mkataba wake wa sasa huko Anfield, uvumi wa PSG umeibuka tena.

Gazeti la L'Equipe limesema Konate anatakiwa na PSG msimu huu wa joto ambao unatarajiwa kuleta mazungumzo juu ya mkataba mpya wa Liverpool.

Konate alipoulizwa kuhusu uvumi huo alisema: "Nimezingatia uwanja na Euro."

"Hata sifikirii hilo. Nimebakiza miaka miwili kwenye mkataba wangu, nina furaha Liverpool."

"Niliona habari za PSG niache peke yangu!" alicheka.

"Mimi ni Mfaransa. Kusikia PSG wana nia kunanifanya nisiwe moto wala baridi, kwa sababu sijafanya mazungumzo nao au mtu yeyote. Kwa kweli ninalenga uwanjani. Sizingatii sana.

"Ni jambo la kimantiki kwa sababu nilizaliwa Ufaransa na Paris. Nina kaka sita wakubwa na wote sita wanaishangilia PSG, nadhani, angalau wanne au watano. Tulitazama mechi nyingi pamoja, walinipeleka kwenye uwanja wa zamani na kituo cha mafunzo.

"Kuna historia kidogo na PSG lakini nilitengeneza njia yangu mwenyewe. Nilicheza Sochaux, kisha Leipzig kabla ya Liverpool. Nina furaha."



**HABARI MICHEZO**

## *Diarra achagua kubakia Yanga*

INATOKA UK. 24

huu, amezidiwa na mlinda mlango wa Coastal Union, Levy Matampi, ambaye amepata 'Clean sheet' nyingi zaidi na kuifanya timu hiyo ya jijini Tanga kumaliza kwenye nafasi ya nne katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hata hivyo mapema msimu uliomalizika, Diarra alishindwa kung'ara katika fainali ya Ngao ya Jamii kwenye hatua ya penalti huku Ally Salim wa Simba akiisaidia timu yake kubeba ngao hiyo kwa kudaka penalti tatu.

Yanga inatarajiwa pia kuiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati maarufu Kombe la Kagame ambayo yamerejea na yatafanyika mapema mwezi ujao kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, visiwani hapa.

## Kocha mpya Simba ni huyu

INATOKA UK. 24

iliyopita kutokana na dau kubwa la kumng'oa, lakini sasa anamaliza mkataba," kilisema chanzo chetu.

Kiliongeza aina ya ufundishaji wa kusakata kandanda ndiyo aina ya soka ambalo Simba wanacheza kama falsafa ya klabu yao inavyojitambulisha.

„Huyu jamaa anafundisha kucheza soka la pasi fupi fupi na kasi na kushambulia mithili ya nyuki, kama ilivyokuwa zamani kwa Milovan Cirkovic au Dragan Popadic, mfano unaona Petro de Luanda kwa misimu ya karibuni ilivyokuwa tishio kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema mtoa taarifa.

Kocha huyo aliiongoza Petro de Luanda kufika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambapo ilitolewa na TP Mazembe ya DRC, ilipochapwa ugenini mabao 2-1, baada ya suluhu nyumbani kwao.

Meneja wa Habari wa Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alikiri mchakato wa kumsaka kocha mpya na kusajili wachezaji wapya unafanyika kwa wakati mmoja na kwa umakini.

„Tuna orodha ya makocha wengi sana walioleta maombi yao, wapo watu wanaoshughulika na suala hilo, pia wapo wengine wanaoshughulika na usajili, tukishamaliza mchakato, kila kitu kitawekwa wazi," Ahmed alisema.

# YANGA YAPANIA MAKUBWA MASHINDANO CAF 2024/2025

**Na Faustine Feliciane,** ZANZIBAR

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga ya Dar es Salaam, wamesema wanajipanga imara zaidi ili kuhakikisha wanafanya vyema katika msimu mpya wa mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Yanga imetwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu wa tatu mfululizo, hivyo kwa mara nyingine itaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Msimu uliomalizika, Yanga ilitolewa katika mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini kwenye hatua ya robo fainali.

Ofisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe, aliliambia gazeti hili jana klabu hiyo itajiimarisha kila idara kwa sababu inataka kupata matokeo mazuri katika mashindano yote watakayoshiriki kwenye msimu mpya.

Kamwe alisema wanafahamu mashindano hayo ya ngazi ya vilabu Afrika ni magumu, hivyo hawataki 'kuishia' tena njiani na wanataka kuipa heshima Tanzania.

Alisema pia hawataki 'kushuka chini' kulinganisha na pale walipoishia msimu uliopita ndio sababu ya kupanga kujiimarisha.

„Kila msimu tunakuwa na malengo yetu, tunapanga vizuri kwa ajili ya Ligi ya Mabingwa Afrika, tunataka kufanya vizuri zaidi, tunataka kuonyesha hatukufanya vizuri msimu uliopita kwa bahati mbaya," alisema Kamwe.

Aliongeza hawatarajii kukibomoa sana kikosi chao lakini watakiboresha kwa ajili ya kujiweka katika mazingira mazuri ya kushindana na vigogo wengine wa Afrika.

„Mchezaji ambaye Yanga tunamhitaji hatutamwacha, lakini tutaboresha kikosi chetu kwa mapendekezo ya kocha wetu, tunataka kuwa na Yanga tishio zaidi ya hii, Wana-Yanga watafurahi msimu ujao," alisema Kamwe.

Timu nyingine ya Bara itakayoshiriki katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ni Azam FC iliyomaliza kwenye nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu huku Simba na Coastal Union zenyewe zitawakilisha katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.



Nahodha wa Timu ya Bwiru FC, Eric Mabogo (kulia), akipokea msaada wa jezi ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kuendeleza na kuhamasisha maendeleo ya michezo jijini Mwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Timu nne zapewa vifaa Mwanza

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

KATIKA kuchangia maendeleo ya michezo, timu za Channel Africans, Bwiru, Majengo na Tiger FC zimepokea vifaa vya michezo ikiwa ni sehemu ya 'amsha amsha' baada ya Real Madrid kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Vifaa hivyo vimetolewa na Kampuni ya michezo ya kubashiri ya BetPawa baada ya Real Madrid kuifunga Borussia Dortmund na kutwaa taji la 15 la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mbali ya kugawa vifaa vya michezo, kampuni hiyo pia ilionyesha mechi hiyo bure kwa kuweka screen kubwa ambapo mamia ya mashabiki wa soka walihudhuria katika kampeni yao iliyojulikana kwa jina la Soka Live iliyofanyika kwenye eneo la Kona ya Bwiru.

Meneja Masoko wa BetPawa, Borah Ndanyungu, alisema wameamua kugawa vifaa vya michezo kwa timu za mitaani kwa sababu malengo yao ni kuendeleza mpira wa miguu.

Mbali ya msaada huo, kampuni hiyo pia iliendesha mashindano ambapo Bwiru FC ilitwaa ubingwa na kupewa zawadi ya mbuzi.

„Hii ni moja ya mikakati yetu ya kuhakikisha soka linachezwa maeneo yote na sisi kama wadau wakubwa, tumeamua kuondoa changamoto za vifaa ambapo timu mbalimbali zimeanza kufaidika.

Asilimia kubwa ya watu duniani wanapenda mpira wa miguu, kwa kutambua hilo, kampuni yetu iliamua kuandaa eneo maalumu la kuonyesha mechi ya fainali na kuleta hamasa kwa jamii. Tunashukuru idadi kubwa ya mashabiki walifika na kushuhudia Real Madrid ikitwaa ubingwa wa kihistoria," alisema Ndanyungu.

# Michezo

Jumatatu Juni 3, 2024
Nipashe




Kimmich akerwa na ubaguzi Ujerumani UK. 21

# Diarra achagua kubakia Yanga sc

●●● Kipa huyo afunguka anahitaji kushinda makombe zaidi msimu ujao na...

**Na Faustine Feliciane,**
ZANZIBAR

BAADA ya kuwapo kwa tetesi za kutakiwa na timu nyingine, kipa chaguo la kwanza la Timu ya Taifa ya Mali na Mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, Djigui Diarra, amesema anapenda kuona anabakia na kuendelea kuchukua makombe zaidi akiwa na klabu hiyo.

Akizungumza na Nipashe kabla ya mechi ya fainali ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Azam FC iliyochezwa jana usiku, Diarra, alisema atafurahi sana endapo Yanga itabeba tena taji la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao pamoja na mashindano mengine mbalimbali watakayoshiriki.

Diarra alisema analifurahia soka la Tanzania na angependa kubakia kuichezea timu hiyo ambayo iko chini ya Kocha Mkuu, Miguel Gamondi.

„Nataka kuona Yanga inafanya vizuri zaidi katika mashindano mbalimbali, mimi bado ni mchezaji wa Yanga, hivyo ningependa kuona tunaendelea kushinda makombe," alisema golikipa huyo.

Kuhusu kubakia au kuondoka nchini, Diarra, alisema endapo atapata ofa nzuri zaidi ya inayotolewa na Yanga, anaamini suala hilo litajadiliwa na viongozi wa klabu yake.

„Ikitokea kuna ofa kutoka katika klabu nyingine, viongozi wangu ndio wenye kuzungumza, kwa sasa malengo yangu ni kuifanya Yanga kuwa tishio zaidi Afrika.

Aliongeza Yanga imechangia kwa kiasi kikubwa kupandisha kiwango chake huku ikimsaidia kuitwa katika kikosi cha Mali, ambacho alikiongoza kwenye mechi za Fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika zilizofanyika mapema mwaka huu nchini Ivory Coast.



„Malengo yangu mengine ni kuendelea kufanya vizuri zaidi kila ninapopata nafasi, kiwango changu kiendelee kuwa juu, kuwa bora na vile vile kuendelea kuisaidia Yanga kufanya vizuri katika mashindano ya kitaifa na kimataifa," Diarra alisema.

Nyota huyo alisema anafurahia maisha yake ndani na Yanga na aliongeza ushirikiano walionao wachezaji, viongozi na mapenzi wanayopata kutoka kwa mashabiki wao ndio msingi pekee wa mafanikio.

„Tuko pamoja sana, tunashirikiana na kusikilizana, umoja wetu ndio umesaidia sisi kufanya vizuri katika kila mechi," aliongeza mlinda mlango huyo.

Diarra ambaye amesimama mechi nyingi zaidi kuliko golikipa mwingine wa Yanga msimu

INAENDELEA UK. 23



Mshambuliaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Charles M'mombwa (kulia), akijiandaa kumtoka mchezaji wa Indonesia katika mechi ya kirafiki iliyochezwa mjini Jakarta nchini humo jana mchana. Timu hizo zilitoka suluhu. **PICHA: TFF**

## Kocha mpya Simba ni huyu

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imetajwa iko katika mazungumzo ya kumwajiri Kocha Mkuu wa Petro de Luanda ya Angola, Alexsandre Santos, ambaye ni raia wa Ureno kwa ajili ya msimu mpya wa mashindano unaotarajiwa kuanza mapema Agosti, mwaka huu.

Tayari Petro de Luanda imethibitisha Santos anaondoka klabuni kwao baada ya kuwaongoza kutwaa ubingwa wa nchi hiyo mara tatu pamoja na Kombe la FA mara moja, ingawa haikuweka wazi wapi ataelekea.

Taarifa kutoka ndani ya Simba zinasema Santos ni mmoja kati ya makocha wanaowaniwa na klabu hiyo kwa muda mrefu, baada ya kumkosa misimu miwili ya nyuma na kuangukia kwa Mserbia Zoran Maki, ambaye hakudumu sana ndani ya kikosi cha Wekundu wa Msimbazi.

Chanzo hicho kilisema Santos pamoja na Florentine Ibenge, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), wanapewa nafasi zaidi ya kuchukua mikoba iliyoachwa na Abdelhak Benchikha.

„Kuna majina ya makocha wengi sana, lakini kwa kiasi kikubwa hawa wawili (Santos na Ibenge), mmoja wao anaweza kupewa mkataba na Simba, kwa sababu ya ukaribu na maelewano na viongozi, mwingine uwezo wake wa ufundishaji unaonekana kuwavutia.

Ibenge, pamoja ni kocha mzuri, ana maelewano mazuri na mabosi, yeye na klabu yake na huyu Mreno mabosi wanavutiwa naye kutokana na uwezo wake mkubwa wa ufundishaji, walimkosa misimu miwili

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042